


MATUKIO YAKIDHIHIRISHWA NA UNABII

 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi. Bwana Mungu wetu, Muumba mkuu wa Mbingu na nchi, Ambaye ulimfufua Yesu tena kutoka kwa wafu, na aliye hai pamoja nasi kwa miaka hii elfu mbili, akiishi daima kuthibitisha Neno Lake na kulifanya halisi kwa kila kizazi. Tunashukuru sana kwa ajili ya Uwepo Wake wa Kiungu sasa hivi, tukijua jambo hili, ya kwamba tunalo tumaini hili kuu, ya kwamba baada ya maisha haya kwisha, tunao Uzima wa Milele katika ulimwengu ujao. Asante, kwa ajili ya jambo hili, Bwana. Na lile tumaini, nanga ya nafsi, ambayo ni imara na ya hakika wakati wa tufani. Na tufani zijapo, mawimbi makubwa yakivuma, tunajisikia ya kwamba kwa imani katika Yeye tunaweza kustahimili kila wimbi.

² Mungu, tusaide usiku wa leo tunapokuja kuwahudumia wagonjwa na walio na haja. Tunaomba, Mungu, ya kwamba pasiwepo na mgonjwa ye yote miongoni mwetu tutakapoondoka usiku wa leo. Tunaomba kila mtu aponywe na Nguvu zako za Kiungu, hapa na kila mahali nchini, waliounganishwa kwa simu, jalia kusiwe na mtu ye yote mnyonge atakeyotoka kwenye jengo lo lote ama kusanyiko lo lote usiku wa leo. Roho Wako na awaponye. Jalia lile Jua kuu la haki, lenye kuponya katika mbawa Zake, lichomoze, litume miali ya imani katika kila moyo wanapolisikiliza Neno, waone madhihirisho ya Roho Mtakatifu akiwashuhudia ya kwamba Yeye yungali hai. Twaomba baraka hizi, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

³ Hakika twahesabu haya ni majaliwa makubwa kuwa hapa usiku wa leo, tena, ku—kuzungumza na watu na kuwaombea wagonjwa. Tunataka kuwasalimu wote waliko kwenye maeneo ya—yaliyounganishwa kwa simu kila mahali nchini, tena usiku wa leo. Na kwa hiyo tunaomba ya kwamba Mungu ambariki kila mmoja wenu, tukitumaini ya kwamba wote waliomkubali Kristo asubuhi ya leo watajazwa na Roho Mtakatifu na daima waishi waaminifu na wanyofu Kwake hata maisha yatakapokoma hapa duniani, maisha haya yanayopatikana na mauti. Na basi wao, kwa kufanya jambo hilo, wana Uzima wa Milele. Hawatakufa katika ule wakati ujao, kwenye wakati mkuu utakaokuja, kwenye ule wakati Mkuu ambao sote tunautazamia.

⁴ Sasa tutasema, wakati nawazia jambo hilo, sio kukatiza. Ndugu Vayle yuko hapa, na huenda nisimwone. Nitaninii... Hivi naweza kukutumia yale makaratasi yenye maandiko ya mkono nitakaporudi Tucson? Ninachunguza, bado sijayasoma yote, nami nitayatuma niyarudishe kwako mara nitakapofika Tucson.

⁵ Sasa ninataka kutangaza jambo fulani. Hii hasa ni kwa ajili ya makanisa kila mahali, hasa huko Magharibi, ama po pote pale kwa wale wanaotaka kuja. Ndugu yetu mpendwa, Ndugu Pearry Green, pamoja na...Ni mtu ambaye ndiye mwanzilishi wa kuunganishwa huku kwa simu hapa. Bwana amekuwa akiliweka moyoni mwake kuja kutuzuru huko Tucson, na kuanzisha ufufuo huko Tucson, ambao kweli tunauhitaji sana. Naye Ndugu Pearry atakuwa huko Tucson. Kama ukitaka kumpata, wasiliana tu na afisi yetu kule. Itakuwa Agosti 10, 11, 12, na 13. Limekuwa moyoni mwake kwa muda mrefu, nami nilimwambia kuna “njia pekee ya kuliondoa moyoni mwako, nenda kalitekeleze.” Naye ni ndugu Mkristo, mtumishi halisi wa Mungu. Nanyi watu, huko Tucson, najua mtabarikiwa atakapohubiri mahali fulani huko, labda kwenye Hoteli ya Ramada ama mahali po pote pale Bwana atakapoandaa, yeye hajapaandika hapa. Lakini ninajua mkija mtabarikiwa, kumsikiliza Ndugu Green akituhubiria Neno la Mungu, labda kuwaombea wagonjwa, ama kufanya cho chote kitakachosababishwa na upako wa Mungu.

⁶ Tunataka pia kumshukuru Ndugu Orman Neville, Ndugu Mann, kwa ajili ya wakati huu mzuri sana wa ushirika pamoja nao. Jinsi nilivyo na shukrani sana kuwa na nani, kuhusika na mtu kama Ndugu Neville, Ndugu Mann, na wahudumu hawa wengine wote hapa. Ninafikiri wamekwisha julishwa. Iwapo hamjajulishwa, na halmashauri yetu na kanisa letu hapa, nina hakika ya kwamba Mungu anawatambua hapa kama watumishi Wake. Bwana na azidi kuwabariki.

⁷ Sasa, niliulizwa jambo fulani dogo hapa, kwenye karatasi ndogo niliyopewa, kuninii...Wao walifanya mkutano wa wadhamini usiku wa juzijuzi hapa, kwenye halmashauri ya wadhamini na mashemasi, nami ninafikiri muhtasari ulisomwa asubuhi ya leo mbele ya kanisa. Jambo ambalo, ndiyo kawaida yetu kufanya hivyo. Katika maamuzi yaliyofanywa na halmashauri ya wadhamini na mashemasi hapa kanisani, bila shaka, hayawezi kumfurahisha kila mtu. Hatuwezi kufanya hivyo. Mimi sihusiki na cho chote cha halmashauri ya wadhamini ama na halmashauri ya mashemasi. Hata sina kura yo yote isipokuwa waende sare, nami sina budi kuwa hapa kufanya jambo hilo wakati huo, Ndugu Orman Neville huchukua kura hiyo ya pili. Ndipo hatuna budi kutia sahihi haya, kwa sababu sisi ni sehemu ya kanisa. Lakini yale halmashauri ya wadhamini na hayo maamuzi wanayofanya ya halmashauri, sisi bila shaka tunayaunga mkono mia kwa mia, kwa maana hiyo ndiyo sababu ya wao kuwa hapa. Na maamuzi yao ni kati yao na Mungu. Mimi siwezi, siwezi na nisingeweza, kwa namna yo yote, kupinga uamuzi huo. Na jambo jingine, ninakatazwa na Serikali ya Marekani kufanya uamuzi wo wote kuhusu jambo hilo, kwa hiyo tafadhali msiniombe kusahihisha maamuzi yao. Mimi siwezi kufanya jambo hilo, na sitasikiliza jambo lo lote juu yake.

Mnaona? Kwa hiyo msiniombe kusahihisha maamuzi yao. Wewe ione halmashauri, hiyo ndiyo iliyotoa maamuzi hayo. Vema.

⁸ Sasa kuhusu mkutano ujao, inawezekana, Bwana akipenda, nitarudi hapa kati ya majuma manne na majuma sita, ama kitu kama hicho, labda kwa ajili ya mkutano wa Jumapili nyingine. Nami nilitangaza asubuhi ya leo nilitaka kuzungumza juu ya *Mungu Amedhihirishwa Katika Neno Lake*, na sitakuwa tu na wakati usiku wa leo, na, kwa kweli, karibu sina sauti ya kutosha kufanya jambo hilo. Na halafu kundi la watu, idadi ya walio nje ni karibu kama na ya walio ndani, na, labda ni zaidi, tukihasabu hayo mabasi na mapikapu na vyombo vilivyojaa watu huko nje. Umefunguliwa, mtambo mdogo wa kurushia matangazo umeongeza sauti kidogo, tunaweza kusikia. Haya mawimbi madogo, mawimbi ya masafa mafupi kutoka Maskanini, tunaweza kuyasikia kwenye umbali wa majumba mawili ya mji. Na baadhi ya magari mengine yako umbali wa majumba kadha ya mji, milolongo ya magari, huku na huko, na kila mahali mitaani, pande zote za Maskani usiku wa leo. Siamini wakati wo wote, ukiangalia kwa macho, tumewahi kuwa na watu wengi zaidi wamesongamana ndani na kulizunguka kanisa kama tulivyo nao usiku wa leo. Kwa hiyo sisi tunaninii . . . Na wengi, wengi, wengi wanakuja kwa magari tu na kuondoka.

⁹ Kwa hiyo hilo linaonyesha, “Palipo na Mzoga, watakusanyika tai.” Na hebu niwaambieni ninyi usiku wa leo, katika kundi hili dogo la watu, ni kusanyiko la kimataifa. Kwa kweli zaidi ya theluthi mbili za mikoa ya shirikisho imewakilishwa hapa, mbali na mataifa matano ya kigeni, hata na Urusi, na sehemu mbalimbali pote nchini. Huko mbali kufikia Venezuela, huko mbali kufikia Jamaica, sehemu mbalimbali nchini, watu wako hapa, wakiona njaa na kiu ya Mungu. Ni wakati wa ajabu namna gani!

¹⁰ Sasa ninataka, kabla ya kuisoma Biblia, nanyi tafadhalini mniombe sasa. Ni—nitajaribu kuleta Ujumbe mdogo, Bwana akipenda, juu ya kupokea uponyaji wa Kiungu. Kwa kuwa, asubuhi ya leo tulinena juu ya wokovu. Na usiku wa leo tutazungumza kwa dakika chache juu ya kuponya Kiungu, kisha tuite mstari wa maombi na kuwaombea watu. Wakati tunafanya jambo hili, huko nje tunakoungamishwa kwa simu, po pote ulipo, hata huko nje kwenye mabasi na kote kwenye magari, kwenye umbali wa jengo moja ama mawili ya kutoka kwenye Maskani; inapofikia wakati wa kuwaombea wagonjwa, kama huwezi kuingia kwenye jengo . . . Jambo ambalo, huwezi, nina hakika sasa, maana milango kila mahali imesongamana sana, kupita, na hakuna nafasi mahali po pote, kwa hiyo wewe omba na mwekeane mikono ninyi kwa ninyi huko nje. Na hebu kila mhudumu aliyeunganishwa kwa simu usiku wa leo, pia aliombe kusanyiko lake wakati ibada ya kuponya inapoendelea.

Tunaamini ya kwamba Mungu yupo mahali pote, kila mahali. Sasa kabla hatujasoma ama . . .

¹¹ Kabla ha—hatujaomba, tunataka kusoma sehemu ya Neno la Mungu. Nami nilibadilisha Maandiko ya—yangu muda mchache uliopita, kwa sababu nikitaka kubadilisha namna ya mkutano niliokuwa nimeazimia moyoni mwangu kwa ajili ya usiku wa leo, kwa hiyo nimeyabadilisha kidogo; na kwa hiyo ilinibidi kubadilisha Maandiko yangu, si kuyabadilisha, bali kuyaweka katika utaratibu mwingine, wa uponyaji wa Kiungu, ili kwamba—kwamba watu wangepahamu.

Hebu na tufungue Luka Mtakatifu, sura ya 24. Na tutaanza kwenye aya ya 12 ya sura ya 24, na kuendelea kusoma mpaka karibu na ya 34. Ni juu ya kufufuka kwake Bwana Yesu.

Lakini Petro, Petro aliondoka akaenda mbio hata kaburini, akainama akachungulia ndani, na akaviona vile vitambaa vya sanda . . . akiyastajabia yaliyotukia.

Na, tazama, siku ile ile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili.

Sasa, vipimo kumi ni—ni maili moja, kwa hiyo ilikuwa kama maili sita.

Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo . . . yote yaliyotukia.

Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao.

Macho yao yakafumbwa wasimtambue.

Akawaambia, Ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea? Wakasimama wamekunja nyuso zao.

Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je! wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo siku hizi?

Akawauliza, Mambo gani?

Sasa kumbukeni, huyu ni Yesu Mwenyewe, aliyefufuka, anazungumza.

Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote;

. . . jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia . . . ka—katika hukumu ya kufa, na wakamsulubisha.

Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboha Israeli. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo;

Tena, wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha, waliokwenda kaburini asubuhi na mapema,

Wasiuone mwili wake; wakaja wakasema ya kwamba wametokewa na malaika waliosema . . .yu hai.

Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyosema, ila yeye hawakumwona.

Sikilizeni sasa; Yesu.

Ndipo yeye akawaambia, Enyi msiofahamu . . .wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii.

Je! haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?

Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza wao yote katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.

Wakakaribia kile kijiji walichokuwa wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele.

Wakamshawishi wakisema, Kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa nao.

Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa.

Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao.

Wakaambiana, Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?

Wakaondoka saa ile ile wakarejea Yerusalemu, wakawakuta wale kumi na mmoja wamekutanika, wao na wale waliokuwa pamoja nao.

Wakisema, Bwana amefufuka kwelikweli, naye amemtokea Simoni.

Nao waliwapa habari ya mambo yale ya njiani, na jinsi alivyotambulikana nao katika kuumega mkate.

¹² Sasa hebu na tuombe. Baba mpenzi Mwenye Rehema, tunakushukuru kwa ajili ya Neno Lako, kwa kuwa Neno Lako ni Kweli, Neno Lako ni Uzima. Nawe, Ee Bwana, na Neno Lako ni Mmoja. Kwa hiyo tunaomba usiku wa leo, Bwana, ya kwamba utakuja miongoni mwetu katika nguvu za kufufuka Kwako na utatuonyesha usiku wa leo, kama wale waliotoka Emau, ya kwamba sisi pia tungerudi manyumbani mwetu, tukisema, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?" Tujalie, Bwana, inaelekea wakati wa jioni tena. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

¹³ Sasa nataka kuzungumza kuhusu Biblia hii. Na somo langu usiku wa leo, somo lenyewe, ni: *Matukio Yakidhihirishwa Na Unabii. Matukio Yakidhihirishwa Na Unabii.*

¹⁴ Sasa, Biblia ni Kitabu tofauti na vitabu vingine vyote vitakatifu. Biblia ni Kitabu tofauti. Ni Kitabu cha unabii, kinachotabiri matukio ya wakati ujao. Na pia Hicho ni Ufunuo wa Yesu Kristo. Kutoka Mwanzo mpaka Ufunuo, kinamleta katika utimilifu Wake, kile Yeye alichokuwa na kile alichu. Na Kitabu chote kizima, Ufunuo 1:1 hadi 3, Kitabu hicho kilisema ni Kitabu cha “Ufunuo wa Yesu Kristo,” ambacho ni Neno la Mungu. “Ufunuo wa Yesu Kristo,” Neno la Mungu!

¹⁵ Sasa, vitabu vingine vyote, vitabu vitakatifu, ni sheria za maadili tu, sheria za kuishi maisha mema, ama kanuni za theolojia. Kitu ambacho... Ni wangapi walipata kusoma Kurani, ile Biblia ya Waislamu, na—na kitabu cha Wabudha, na kadhalika? Ni orodha tu ya kanuni za maadili, jinsi watu wanavyopaswa kuishi, jinsi wanavyopaswa kuishi, lakini hakitabiri, hakisemi jambo lo lote kuhusu mambo haya ama juu ya karama yo yote maalum kutolewa kwa mtu ye yote, jambo lo lote litakalotukia. Ni kama tu kujiunga na loji ama kitu fulani. Kwa hiyo, wakati makanisa yanapofikia mahali ambapo wanafanya kanisa lao loji tu ya kujiunga nayo, basi wametoka moja kwa moja kwenye Neno la Mungu.

¹⁶ Kwa maana Biblia ni ushuhuda hai, uliotabiriwa wa Yesu Kristo. Na kama vile dunia imekua katika utimilifu wake, na pia mizabibu inakua na kukomaa, siku zinakua katika utimilifu Wake, Biblia ilidhihirishwa katika ukamilifu Wake katika Utu wa Yesu Kristo. Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililofunuliwa, kitabu chote kizima cha ukombozi. Biblia ni Neno la Mungu, linalotabiri matukio ya baadaye. Waamini wake wanaamriwa na Mwandishi Wake kusoma na kuamini kila Neno Lake, si sehemu Yake tu. Neno moja, kutoliamini, wewe afadhali uache kujaribu hata utakapoliamini hilo Neno. Kila Neno ni sehemu ya Mwenyezi Mungu kabisa; Mungu aliyedhihirishwa, aliyefunganishwa katika Neno Lake, apate kuonyesha Yeye ni Nani. Tunaamriwa, kama waamini, kuamini kila Neno Lake. Nalo limeandikwa na Mwandishi wa Mungu Mwenyewe. Hakuna mtu anayeweza kuongeza cho chote Kwake ama kutoa cho chote Kwake. Kama ungefanya hivyo, ungekuwa mwili kioja wa Mungu. Ungekuwa, labda kama vidole sita kwenye mkono mmoja, ama—ama mikonu mitatu, ama kitu fulani, kuongeza kitu fulani, kutoa kitu fulani kwake na kupungukiwa na mkono mmoja, kupungukiwa na kidole kimoja. Ni Mwili mkamilifu wa Yesu Kristo. Na katika Kristo, akiwa Mwanamume, Bwana Arusi, Bibi-arusi amewakilishwa ndani Yake pia. Na hawa wawili ni Mmoja.” “Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu nanyi ndani Yangu.” Ni picha kamilifu jinsi gani!

¹⁷ Na waamini wa kweli katika Neno hili, wanaolikubali namna hiyo, huliadini, na kwa saburi hukingojea ahadi Zake zilizotabiriwa, kila moja ya hizo kudhihirishwa katika wakati wake. Kila mwamini amelitazamia jambo hilo. Kila mwamini ambaye amekuwa macho, akitazamia, ndiye ambaye kwake Hilo limefunuliwa.

¹⁸ Sasa angalieni katika siku za kuja kwa Bwana Yesu. Kwa nini watu hao hawakumtambua Yohana, wakati Biblia ilisema dhahiri kwa Isaya, “Kutakuwako na sauti ya mtu aliaye nyikani, ‘Itengenezeni njia ya Bwana’”? Nabii wao wa mwisho waliyekuwa naye, ambaye ni Malaki 3, alisema, “Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu kuitayarisha njia.” Kwa nini wao hawakuona jambo hilo? Ni kwa sababu walikuwa wakitazamia kitu fulani kilichokuwa kimefanywa, wakiweka msingi mawazo yao juu ya ujumbe fulani uliokuwa umetangulia, nao wakashindwa kuona dhihirisho la wakati uliopo la Mungu katika siku waliyokuwa wanaishi.

¹⁹ Na Wakristo, kila mahali, hapo ndipo ulimwengu unaposimama hasa usiku wa leo. Bila ya ubishi, hiyo ni kweli! Wakristo, kila mahali, wanajaribu kuangalia nyuma kwenye kanuni fulani za maadili ambayo Bw. Luther aliandika, ama Bw. Wesley, Sankey, Finney, Knox, Calvin; ambao, hakuna mmoja wetu anayeweza kuyanenea mabaya, lakini hiyo ilikuwa ni katika siku iliyopita.

²⁰ Mafarisayo walitazama nyuma kuona yale aliyosema Musa, nao wakasema, “Tuna Musa. Hatujui unakotoka Wewe.”

²¹ Lakini kumbukeni wakati Musa hapa, wao hawakujua alikotoka. Mnaona? Na sasa wao... Si ajabu Yesu aliwaambia, “Mnayapamba makaburi ya manabii, nanyi ndinyi mliowaweka mle.” Baada ya Ujumbe wao kwisha! Ujumbe unapita, watu wanauona, wanaufanyia mzaha (ulimwengu unaufanyia mzaha.) Na baada ya huyo mjumbe kumaliza na Ujumbe kumalizika, ndipo wao wanajenga madhehebu juu ya Ujumbe huo. Na hapo wanakufa, papo hapo, hawafufuki tena.

²² Angalia kwa kitambo kidogo tu, kwa baadhi yenu enyi watu, na hasa sana ninazungumza na ninyi Wakatoliki. Hivi mnatambua, hivi mmewahi kusoma historia yenyewe, historia yenu ya kanisa Katoliki la Kirumi? Jinsi ambavyo kwenye historia ya wafia imani, tangu Mtakatifu Agostino wa Hippo, ni watu milioni ngapi wasio na hatia ambao waliuawa na kanisa! Ninasahau, siwezi kukumbuka idadi kamili, lakini imefikia kwenye mamilioni, tangu Mtakatifu Hippo wa... Mtakatifu Agostino wa Hip-... wa Hippo, Afrika, alipotoa tangazo ya kwamba ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kabisa kumwua ye yote ambaye analipinga kanisa Katoliki la Kirumi. Hivi mnatambua ya kwamba katika jambo hilo, kwamba Mtakatifu Patrick hakutambuliwa mpaka baada ya kufa kwake, kama Mkatoliki wa Kirumi? Yeye alipinga papa na matendo yake yote, na

kanisa Katoliki lenyewe likawaua makumi elfu ya watoto wake. Hivi mlijua ya kwamba kanisa Katoliki lilimwua Joan wa Arc, yule maskini mwanamke mtakatifu, wakamchoma moto, kwa ninii. . . wakasema yeye ni mchawi. Miaka mia mbili baadaye, wakachimbua miili ya hao makasisi, walipotambua ilikuwa ni makosa, na kuitupa baharini, bila kuwazika kweye ardhi iliyowekwa wakfu, ili kufanya kitubio.

Usiache siku hii ipite juu ya kichwa chako, kisha uwe mjinga.

²³ Jinsi hao makasisi wangetaka, usiku wa leo, kuja, hao waliomhukumu Yesu. Jambo pekee, wao hawakuona ubashiri wa saa hiyo. Kama wao. . . Yesu alisema, “Mwayachunguza Maandiko, kwa maana ndani Yake mnafikiri,” ama kwa maneno mengine, “mnadai kwamba mna Uzima wa Milele, na Maandiko hayo ndiyo yanayowaambia Mimi ni Nani,” kwa ajili ya saa hiyo.

²⁴ Angalieni, Biblia haiwezi kushindwa. Ndilo jambo moja Hiyo haiwezi kushindwa, Neno la Mungu kushindwa, kwa maana Hiyo hutabiri matendo ya Mwandishi Wake kabla Yeye hajafanya jambo hilo.

²⁵ Sasa, kuna nafasi moja kati ya elfu ambapo mtu anaweza kubashiri ya kwamba jambo fulani litatukia, nalo lingetukia. Lakini basi kama akiweka *mahali* litakapotukia, hilo linampunguzia kufikia labda nafasi moja kati ya elfu kumi. Kama akisema *siku* litakapotukia, hilo linaipunguza, nafasi moja kati ya kama milioni moja. Na litatukia kwa *nani*, hilo linaipunguza kufikia nafasi bilioni kadha.

²⁶ Lakini Biblia hii inawaambia hasa ni *nani, ni lini, ni wapi*, na ni kitu *gani* cha kutazamia, na wala haijashindwa hata wakati mmoja. Kwa hiyo, katika majadiliano mafupi si muda mrefu uliopita, nikiwa na kasisi wa kanisa la Moyo Mtakatifu hapa; yeye akasema, “Bw. Branham, unajaribu kuibishania Biblia.” Kasema, “Hiyo ni historia ya kanisa.”

Nikasema, “Hiyo si historia. Ni Mungu, Mwenyewe, katika maandiko.”

Akasema, “Mungu yuko ndani ya kanisa Lake.”

²⁷ Nikasema, “Mungu yuko ndani ya Neno. Na cho chote kilicho kinyume Chake, na kiwe uongo. Kwa maana Yeye alisema, ‘Neno Langu na liwe kweli na kila neno la mwanadamu uongo.’”

Akasema, “Haitupasi kubishana.”

²⁸ Nikasema, “Mimi sikukuomba ubishane, lakini Biblia inasema, ‘Njoni, tusemezane.’” Mwajua.

²⁹ Inatabiri matendo ya Mwandishi kabla Yeye hajayatenda. Kwa hiyo, kusema hilo, basi hilo linamweka kila mwanamume na mwanamke, mbele ya Kiti cha Hukumu, bila udhuru wo wote. Kama ukichukua asemalo Mmethodisti kuhusu Hilo,

kile Mbatisti asemacho juu ya Hilo, kile Mkatoliki asemacho, kile Mpentekoste anachosema, ama kanisa lingine lo lote, huenda ukawa na masikitiko fulani kwenye ile Hukumu. Lakini kama utaangalia tu lile Biblia inalosema litatukia, na ni lini litakapotukia, basi utatambua kinachotukia.

³⁰ Sasa, si dhahiri moja kwa moja kwamba watu wote wanaweza kuliona, kwa kuwa Yesu alimshukuru Mungu kwa ajili ya kulificha wenye hekima na akili, na angelifunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza. Wazia juu ya Mwenyezi Mungu akiketi kwenye Neno Lake Mwenyewe, akiwa na nguvu za kuwapofusha matajiri na wajuvi na—na wanachuoni wenye elimu, akawapofusha macho yao wasiweze kumwona Yeye, kisha anayafungua macho ya maskini na wasiojua kusoma.

³¹ Angalia watu hawa kutoka Emau, Yeye alisema u— ufahamu wao Kwake ulizuiwa. Wao walizungumza Naye wala hata hawakujua Yeye alikuwa ni nani, siku nzima. Mungu anaweza kufanya jambo hilo, kwa kuwa Yeye ni Mungu.

³² Hivyo ndivyo hasa alivyowafanyia hao makuhani, hao waandishi, kwa sababu ilikuwa imeandikwa ya kwamba ilimpasa Yeye kufanya jambo hilo. Mungu aliyapofusha macho yao ili kwamba tupate nafasi. Angalia, wao wasingeweza kuona, haidhuru walikuwa wasomi namna gani, walikuwa makuhani namna gani, yale waliyokuwa wamefanya, bado wasingeweza kuliona Hilo, kwa maana walikuwa vipofu. Macho yao huenda yalikuwa ishirini kwa ishirini, kimwili. Lakini ni macho yao ya rohani!

³³ Nilikuwa nikijaribu kusema jambo lilo hilo asubuhi ya leo juu ya uzinzi wa wanawake, wakivalia jinsi wanavyovalia sasa. Wao ni wazinzi. Katika Kitabu cha Mungu wao wana hatia ya uzinzi kila wakati wanapovaa nguo zao zinazoonekana za kizinzi. Nafsi yao, bila kujua hilo. Ninaaamini hao wanawake, wengi wao, maelfu yao, hawana hatia, wala wasingeweza kamwe kufanya uzinzi. Na maskini wanawake hao, wakiwa na mtu atakayewaruhusu wafanye jambo hilo, bila kuliweka hadharani na kusema kweli, wanatenda uzinzi. Jambo ambalo, Biblia ilisema, “Kahaba aliyeketi juu ya maji mengi, ya kwamba wafalme wote wa duniani na watu wa duniani, makanisa na kadhalika, walifanya uasherati pamoja naye. Naye alikuwa MAMA WA MAKAHABA,” madhehebu.

³⁴ Tunaiangalia Biblia, kwa maana Mungu hatuachi katika giza. Aliituma Biblia kututabiria matukio kabla hayajatukia, na hali yenyewe hasa na wakati yatakapokuja.

³⁵ Sasa, ni kitu kama kuangalia kwenye kalenda kuona ni tarehe gani. Kama ukifikiria, useme ya kwamba hii ni, “Je! hii ni Jumamosi, Jumapili, ni siku gani?” Angalia kwenye kalenda. Kalenda itakwambia ni siku gani. Unapoono matendo ya watu, labda wakienda kanisani, unaona ni—ninii . . . unasikia kengele

zikilia, hujui ni siku gani. Angalia kwenye kalenda, itakwambia ni siku gani.

³⁶ Na mnapoona kanisa likiwa la kilimwengu, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, mkiona ulimwengu wote wa makanisa ukiingia katika ninii...kuabudu “mungu wa kizazi hiki kiovu,” na kuona jambo hilo; halafu mkiona kundi dogo la walio wachache limekusanyika chini ya upako wa Mungu, likidhihirisha tena Maisha ya Yesu Kristo, kwa Maandiko yanayopaswa kutukia, mnaajua mnaishi wakati gani.

³⁷ Biblia hii inatabiri, kwa unabii, ni siku gani tunayoishi, na wakati gani tunaishi, na ni matukio ya namna gani yanayopaswa kutukia. Inatabiri jambo hilo kikamilifu kabisa, wala haijakosea hata kizazi kimoja, wakati wote. Hakuna hata wakati mmoja ambapo imekosea, wala haitakosea, kwa kuwa waliochaguliwa tangu zamani kuliona wataliona. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba Yangu watakuja.” Ni Neno likiungana na Neno. Haliwezi kutenda vinginevyo. Tunajua jambo hilo, siku tunayoishi.

³⁸ Lakini kama vile ilivyokuwa katika kila wakati, watu wanamwachilia mtu aweke tafsiri yao kwenye Neno hili, na inawafanya watu wasione matukio yaliyotukia. Jambo lile lile limefanyika kwa Mafarisayo na Masadukayo. Hata wakati Paulo aliposimama pale na kujaribu kuyanukuu Maandiko, na mtu mmoja akampiga kofi usoni kwa sababu alimwita kuhani mkuu ukuta uliopakwa chokaa. Ndipo basi wakakosa kumwona Mungu akithibitisha Neno Lake lililotabiriwa.

³⁹ Mnaona, Biblia haijipingi Yenyewe; Biblia ni Mungu. Hakuna kuhitilafiana kwa Mungu; Yeye ni mkamilifu.

⁴⁰ Lakini watu, kwa ufasiri wao wenyewe! Sasa angalia, hebu niwaonyeshe, enyi marafiki. Makanisa hayawezi kukubaliana juu ya fasiri Yake. Mmethodisti hawezi kukubaliana na Mbatisti, Mbatisti hawezi kukubaliana na Mpresbiteri, Mpresbiteri na Wapentekoste. Na kukiwepo na kama madhehebu arobaini ya Wapentekoste, wao hawawezi kukubaliana wao kwa wao. Kwa hiyo unaona, hiyo ingekuwa ni Babeli tena, mchafuko.

⁴¹ Lakini Mungu hujifasiria Mwenyewe Neno Lake. Yeye aliahidi jambo hili, na halafu analifanya Mwenyewe. Hutoa, Yeye Mwenyewe, fasiri Yake, kwa maana Yeye hujitambulisha Mwenyewe katika saa hiyo. Ni mbali jinsi gani Mwi—Mwili wa Kristo umekwenda, kutoka miguuni mpaka kichwani!

⁴² Angalia, basi hiyo ndiyo sababu ambayo watu hawa wanakosa kulipata, kwa sababu wao husikiliza kile mtu mwingine anachosema juu Yake, badala ya kulisoma Neno kama Yesu alivyowaambia wafanye, “Na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Yachunguzeni Maandiko, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo

yanayonishuhudia.” Kwa maneno mengine, sikilizeni, “Ati nini? Someni Maandiko na mwone yale Masihi aliyopaswa kufanya. Mwone ni wakati gani Masihi alipaswa kuja. Angalieni ni nani aliyekuwa amtangulie Masihi. Angalia hiyo saa. Kunapaswa kuwe na sauti iliayo nyikani, Yohana. Nanyi mmentendea sawa na mlivyotaka. Angalieni yale ningalipaswa kufanya nitakapokuja. Na sasa mmefanya nini? Hivi nimekosa kutimiza jambo Hili?” Mnaona, Yesu akinena, “Hivi nimeshindwa kutimiza jambo hili?”

⁴³ Angalia, tulipopitia Maandiko alasiri ya leo, jinsi ambavyo kila kitu kilichotabiriwa kumhusu Yeye kilivyotukia vile vile kabisa jinsi kilivyopaswa kutukia. Wao walipaswa kujua tukio hili. “Huyu mshupavu wa dini, kijana aliyeinuka, mwenye umri wa kama miaka thelathini na mitatu na . . . ama miaka thelathini, na akashuka kwenda kule chini na kudai kila namna ya Nuru, na Hua wakipanda. Na, mbona, ilikuwa tu ni fe—fedheha.” Wakasema, “Yeye alizaliwa na wazazi haramu, akadai alizaliwa na bikira.”

⁴⁴ Hivi hawakupaswa kujua ya kwamba Isaya alisema, katika Isaya 9:6, “Kwa maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa”? Hivi hawakupaswa kujua pia ya kwamba nabii Isaya alisema, “Bikira atachukua mimba”? Walipaswa kujua mambo haya. Lakini, mnaona, jambo lenyewe lilikuwa kwamba, wao walikuwa wakiliweka mahali fulani huko mbele. Naye Mtu huyu, kwao, hakutimiza zile sifa. Lakini Yeye aliwaambia, “Chunguzeni Maandiko, kwa maana mnafikiri ndani yake kwamba mna Uzima wa Milele, nayo Ndiyo jambo lenyewe hasa linaloshuhudia Ujumbe Wangu.” Si yale wanatheolojia fulani waliosema; bali yale Mungu, Neno Lake Mwenyewe, liliyosema yangetukia! Amina!

⁴⁵ Hivyo ndivyo ilivyo leo! Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa Hayo ndiyo yanayotwambia saa tunayoishi, yanatwambia hasa yale yatakayotukia katika siku hii. Hayo ndiyo unayopaswa kutegemea, kwa kuwa Hayo ndiyo yanayoshuhudia juu ya Utu wa Yesu Kristo. Kwa kuwa Biblia ilisema, ya kwamba, “Ni Yeye yule jana, leo, na hata milele,” maana Yeye ni ufunuo wa Neno katika huo wakati. Hawezi kuwa tofauti.

⁴⁶ Kwa hiyo kwa kusikiliza tafsiri ya mwanadamu, wao wanaona thibitisho la Neno la Mungu likitimizwa, wanashindwa kulitambua. Kwa sababu, linasonga mbele wakati wote, lakini kwa sababu wao wanasikiliza . . . Naye Yesu alisema, “Wao ni viongozi vipofu.” Na kama kipofu akimwongoza kipofu, kitu gani kinawatukia? Sasa kumbukeni, Biblia ilitabiri ya kwamba wakati huu wa kidini wa Wakati huu wa Laodikia ulikuwa kipofu. Walikuwa wamentupa nje ya kanisa. Hakuna wakati mwingine, wakati mwingine wa kanisa, ambao Yesu alikuwa nje. Isipokuwa wakati wa kanisa la Laodikia, Yeye alikuwa nje, akijaribu kurudi kuingia ndani, “Ninasimama mlangoni

nikibisha.” Yeye anapaswa kuwa yuko ndani. Lakini Yeye alisema, “Kwa sababu unasema ‘Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, sina haja na kitu,’ nawe hujui, hujui ya kwamba wewe ni kipofu, anayeongoza kipofu, maskini wa roho, mnyonge, mwenye mashaka, uchi, nawe hujui.” Ni ninii jinsi gani. . . Kama mtu alikuwa yu uchi barabarani, mwenye mashaka, kipofu, naye alijua alikuwa na akili ya kutosha hata ungemwambia yeye alikuwa uchi, yeye angejaribu kufanya jambo fulani juu ya jambo hilo. Lakini wakati anapotikisa kichwa chake, aseme, “Sitasikiliza jambo Hilo. Wewe ni nani ati uniambie la kufanya? Najua ninaposimama.” Sasa, kama hiyo si hali ya kusikitisha, sijui. Na hilo ndilo hasa ambalo Mungu wa Biblia hii alilosema ya kwamba kanisa lingekuwa nalo, katika kizazi hiki kiovu sasa hivi, katika wakati wa mwisho wa kanisa ambamo tunaishi.

⁴⁷ Angalia, lakini kwa watu, “Kila nimpendaye, ninamkemea.” Sasa, kama ukikemewa na Bwana, kwa yale unayofanya, toka kwenye jambo hilo basi! Liache. “Kila nimpendaye, ninamkemea.”

⁴⁸ Sasa, kumwona Mungu, sasa, vipi kama hao Mafarisayo wangalisema, “Ngoja kidogo. Mtu huyo ametusai kwelikweli, Yeye amesema, ‘Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele; Hayo ndiyo yanayonishuhudia.’ Afadhali niangalie nyuma kwenye Maandiko na kuona yale anayopaswa kufanya, Yeye ni Nani, yale yanayopaswa kutukia. Ninapaswa nirudi kuangalia na kujua”? Badala ya jambo hilo, wao waliwaendea makuhani na kuwauliza, “Vipi juu ya jambo Hilo?” Mnaona hiyo tofauti yake? Wao walipaswa kuwa wanasoma Neno.

⁴⁹ Katika Waebrania 1:1, Biblia ilisema, “Mungu, katika zamani nyingi,” yaani, “zamani na kwa njia nyingi aliandika Biblia kwa manabii.” Sasa angalia, Yeye aliandika Biblia kwa njia Yake Mwenyewe aliyojichagulia. Mnaona? Sasa, haikumbidi kuiandika namna hiyo, wala haikumbidi kumwoko mwanadamu kwa Damu. Haikumbidi kuihubiri Injili kwa njia ya mwanadamu; Yeye angeliacha jua ama mwezi ama nyota zihubiri Injili, angeuacha upepo uvumishe Injili. Lakini Yeye alimchagua mwanadamu! Naye alichagua njia ile Neno Lake lilivyokuja, na hiyo ilikuwa kwa manabii Wake ambao walichaguliwa tangu zamani na kutengwa tangu zamani, wakiwa sehemu ya Neno la Mungu, wakitangaza ufunuo wa Neno Lake kwa wakati huo na majira hayo. “Kwa kuwa Neno la Mungu liliwajilia manabii peke yao.” Haliji kwa mwanatheolojia kamwe. Nionyeshe Maandiko. Linawajilia manabii peke yao. Mungu hawezi kusema uongo. Kwa hiyo Mungu aliandika Biblia kwa njia aliyochagua Yeye Mwenyewe, na manabii Wake aliowachagua Mwenyewe; si manabii waliochaguliwa na mwanadamu, bali manabii waliochaguliwa na Mungu.

⁵⁰ Ndipo waamini wake hutazamia kutimizwa kwa yale nabii wao alivyosema, na hilo ndilo utambulisho ya kwamba wao ni manabii wa Mungu. Kwa sababu, kwanza, wao wametiwa upako. Halafu, wao wanadumu kikamilifu na Neno la wakati huo. Basi hivyo ndivyo vitambulisho vyake. Mnaona, tulipitia hayo Jumapili iliyopita. Manabii wengi wa uongo watainuka. Nasi tulitoa mifano ya jinsi ambavyo Balaamu na Musa, wote wawili wametiwa mafuta na Roho yule yule, mmoja wao alisema, “Sisi sote ni kitu kimoja. Hebu tuje tuungane, tuwachanganye wasichana wetu na watu wote pamoja. Tuna wasichana wazuri hapa, na ninyi wavulana njoni huku mkajitwalie mke mzuri. Hilo ni sawa, sisi sote ni jamii moja ya watu, hata hivyo, ni jamii ile ile.” Mungu kamwe hakuwasamehe kwa ajili ya jambo hilo. Wao walisikiliza hayo.

⁵¹ Mnaona, ulimwengu na wa—watu wanatazamia mwanya fulani mdogo, njia ndogo ya kando, njia fupi ya mkato, bali hakuna njia za mikato katika Neno la Mungu. Kuna Mtindo mmoja. Huna budi kujikata mwenyewe na kulingana na Mtindo huo, si kujaribu kukata Mtindo huo kusudi ulingane na wewe. Kila mtu hana budi kufanya jambo hilo. Hiyo ndiyo njia pekee aliyo nayo Mungu ya kufanya jambo hilo.

⁵² Angalia sasa, waamini hungojea Neno hilo lithibitishwe. Mnaona, Hilo halikuandikwa na mwanadamu, bali na Bwana Mungu, kwa hiyo Hicho si kitabu cha mwanadamu.

⁵³ Mtu fulani alisema, “Ni maandishi fulani tu ya kale ya Kiebrania.” Hivi Waebrania wangaliandika waraka ambao uliwahukumumu wao wenyewe? Hivi hilo taifa zuri la Wayahudi, linalojivuna na lililoadibishwa, hivi wao wangeandika makosa yao wenyewe, wakijihukumumu wenyewe? La hasha. Kusema dhambi zake mwenyewe, jinsi walivyoingia katika ibada za sanamu, jinsi walivyofanya uasherati dhidi ya Neno la Mungu? La, la. Wao wasingeweza kusimulia hayo, hilo taifa lenye majivuno.

⁵⁴ Si kitabu cha mwanadamu. Ni Kitabu cha Mungu. Na mtu anayeona maono ama anayesikia Sauti ya Mungu, hawakuielewa (mara nyingi) wao wenyewe, katika hali nyingi. Mnaona? Mwanadamu hakuiandika Biblia. Mungu aliandika Biblia. Si ninii—si kitabu cha mwanadamu, ni Kitabu cha Mungu. Ni mawazo ya Mungu yakielezwa katika midomo ya mwanadamu. Hayo ndiyo yanayoifanya Biblia. Wazo lililotamkwa ni neno. Na hapo mwanzo kulikuwa na wazo la Mungu, akalitamka kupitia midomo ya manabii Wake na kulithibitisha kwa watumishi Wake. Mnaona? Angalia.

⁵⁵ Mungu hujichagua Mwenyewe, kwa kuchagua tangu zamani, akawachagua manabii kwa ajili ya kila wakati. Angalia jambo hilo. Yeye huweka tabia ya huyo nabii ipate kulingana na wakati huo. Mnaona, Yeye huweka mtindo wake, cho chote afanyacho. Yeye humweka kama ana elimu ama hana

elimu. Yeye humwekea vipawa, namna atakavyohubiri, karama atakazokuwa nazo. Na Ujumbe wa wakati huo fulani, Mungu alichagua tangu zamani kitu hicho maalum kitendeke wala hakuna kitu kingine kinachoweza kuchukua mahali pake. Sijali ni nini, ni mafanikio mangapi ya kujitengenezea, hakuna kinachoweza kupachukua mahali pake. Yeye alimchagua mtu huyo tangu zamani labda mtu mjinga, labda Yeye angalimchagua tangu zamani mtu wa aina nyingine. Cho chote alichu, yeye humpa tabaka yake, karama za—zake, anampa tabia yake, mwenendo wake, na cho chote kile, jinsi anavyojieleza, cho chote afanyacho. Yeye humfanya mtu wa wakati huo ili kuwashika watu wa wakati huo. Kweli. Yeye hufanya jambo hilo.

⁵⁶ Kwenye mwisho wa kila wakati, wakati kanisa limegeukia ulimwengu na dhambi, na linaegemea kwenye fasiri ya binadamu ya Neno. Kama kawaida, wao daima, katika mwisho wa wakati, wameingia katika mchafuko kama huo kwa wanatheolojia wao na makasisi mpaka daima ni mchafuko. Daima fasiri yao ni mbaya, hakuna hata wakati mmoja imeshindwa kuwa mbaya. Wala hakuna hata wakati mmoja Neno la Mungu limeshindwa kuwa kweli. Hiyo ndiyo tofauti.

⁵⁷ Sasa unaona, Mungu aliandika Biblia, Yeye Mwenyewe. Sasa, Mungu anaweza kuongea. Musa alisema aliongea Naye. Yeremia alisema, “Yeye aliweka Maneno katika kinywa changu.” Pia Mungu anaweza kuandika. Yeye aliandika zile amri kumi kwa kidole Chake Mwenyewe. Aliandika kwenye kuta za Babeli. Na, kumbukeni, katika Agano la Kale peke yake, mara elfu mbili manabii walisema, “BWANA ASEMA HIVI!” Mungu anaweza kuzungumza, Mungu anaweza kuandika. Bila shaka. Karibu asilimia tisini ya Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, ni Maneno yenyewe ya Mungu Mwenyewe, Yesu Kristo akinena. Kwa hiyo, kama Mungu anaweza kuandika, kama Mungu anaweza kusoma, kama Mungu anaweza kuzungumza, hivi Yeye hawezi kuwafanya wengine wafanye jambo lile lile? Je! Yeye hakumwambia Musa, “Ni nani amfanyaye mtu kuwa bubu ama ni nani anayempa kusema?” Mungu aliandika Biblia kwa manabii, njia Yake ya kufanya jambo hilo.

⁵⁸ Sasa kila wakati ambapo kanisa linapoingia kwenye mchafuko (Naye Mungu alitangulia kujua kwamba wangechafukiwa, kwa sababu Yeye alitangulia kujua mambo yote) kwa hiyo Yeye huwa na nabii Wake fulani tayari kwa ajili ya huo wakati, kuwaita wateule Wake kwa Neno Lake lililothibitishwa la ishara na maajabu, na uthibitisho wa Neno Lake, “akithibitisha lile Neno kwa ishara zilizofuatana nalo,” kama alivyoahidi. Yeye hutoa tafsiri ya kweli baada ya nabii mwenyewe kuthibitishwa.

⁵⁹ Wote ila wale, wale wateule ambao ametumwa kwao, wanamchukia. Sasa, chunguza kila wakati uone kama jambo

hilo ni kweli ama si kweli. Ni wale tu aliotumwa kwao! “Alikuwa Kwake na walio Wake hawakumpokea; bali wale waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu.” Angalia, si . . . kila uchunguzi wa Neno, katika kila tukio, na mwishoni mwa kila wakati ama upeo ama njia panda, kama nilivyohubiri juu ya jambo hilo mara nyingi.

⁶⁰ Angalia wakati wa Nuhu, mwisho kabisa kabla ya hukumu. Ilitukia nini? Nuhu, ni jamaa yake mwenyewe tu ambayo ilimwamini mtu huyo. Hao wengine walimpinga. Na ulimwengu mzima ukaangamizwa.

⁶¹ Katika siku za Ibrahimu, ni kundi tu la Ibrahimu lililoamini. Wakati wale Malaika walipoenda na kuhubiri Sodoma, ni Lutu peke yake na mkewe na binti zake wawili walitoka, na mkewe akageuka akawa nguzo ya chumvi.

⁶² Katika siku za Musa, ni wateule tu wa Israeli waliotoka. Naye Farao alimchukia.

⁶³ Katika siku za Eliya, kila kitu (karibu kila kitu) ila watu elfu saba, kila mmoja wao alimchukia, taifa zima.

⁶⁴ Katika siku za Yeria, mbona, walimtipua matunda mabichi, na kumwita mshupavu wa dini, kwa sababu alilala kwa ubavu wake kwa siku nyingi sana, na kwa ubavu huo mwingine, na—na akachukua vitu na kufanya ishara. Walimchukia.

⁶⁵ Nabii Isaya, yeye alihukumu taifa hilo sana hata wao wakamkata vipande viwili kwa msumeni. Kweli.

⁶⁶ Yohana Mbatizaji, “Yeye alikuwa mtu mwitu kule, mwenda wazimu fulani anayepiga makelele.”

Wote ila—ila hao wanafunzi ambao aliwapeleka kwa Yesu Kristo kama kanisa! Hilo hapo. Yohana aliwatayarisha watu fulani. Yeye alikuwa na wangapi? Ungeweza kuwahesabu kwa vidole viwili . . . mikono miwili, vidole vyako, ni wangapi ambao Yohana aliwapeleka kwa Yesu wakati alipokuja. Sasa, vipi kuhusu Kuja Kwake kwa pili? Wazieni jambo hilo.

⁶⁷ Lakini wakati waamini wa kweli wa Biblia wanapoliona Neno likithibitishwa wazi kwa ajili ya wakati wao, wao wanaamini. Hakuna njia ya kuwatenga na jambo Hilo, wao wanaliamini. Hata wanatia muhuri ushuhuda wao kwa damu yao. Wao wanaliamini. Basi Hilo ni kwa ajili yao, hao waliochaguliwa tangu zamani, ambao wakati fulani ndio waona na kuliamini.

⁶⁸ Wengine hawawezi tu kuliona; wamepofushwa. Sasa, unasema, “Hawawezi kuliona.” Sasa, kama Balaamu, mbona Balaamu hakuweza kuliona Hilo? Yeye alikuwa ni nabii, aliyetiwa mafuta? Kwa nini Farao hakuweza kuliona? Wakati ameona mkono wa Mungu ukishuka na kutenda miujiza humo, jambo hilo liliufanya tu moyo wake kuwa mgumu. Hiyo ni kweli? Kwa nini Dathani hakuweza kuliona, na huku yeye mwenyewe

ni Myahudi? Moja kwa moja huko nje, walikuwa wamevuka Bahari ya Shamu, na wakala mana kila usiku, iliyoanguka mpya, na hata hivyo wasingeweza kuliona. Mbona Kora hakuona jambo Hilo? Kwa nini Kayafa hakuliona? Yeye alikuwa ni mtu mkuu wa dini duniani wakati huo. Kwa nini Yeye hakuona huyo alikuwa ni Masihi? Mbona Yuda hakuliona? Yuda alikuwa wakati wote pamoja nao, akitembea pamoja nao, akifanya miujiza pamoja nao. Bali Neno lilipaswa kutimizwa. Biblia ilisema wao waliinuliwa kupachukua mahali hapo. Waliinuliwa kwa kusudi hilo. Hiyo ni kweli. Warumi 8 inasema hivyo.

⁶⁹ Sasa waamini wanaweza kuona Neno likifanyika mwili katika kizazi chao, Mungu akinena. Sasa, hao waamini halisi na wa kweli, hao elfu saba (ama walikuwa mia saba?) katika siku za Eliya. Eflu saba ndiyo sahihi. Katika siku za Eliya, kulikuwako na watu elfu saba kati ya watu kama milioni mbili ama tatu, walioona ya kwamba jambo Hilo lilikuwa kweli. Na si moja ya mia ya hao watu, hata. Lakini wao waliona kwamba Hilo lilikuwa ni kweli. Walimwona Mungu amedhihirishwa. Maskini yule mjane ambaye Elisha alitumwa kwake, yeye alienda kuokota zile kuni, kutengeneza mkate, na wa kutosha tu kutengeneza mkate wake na wa mwanawe, kisha wafe. Lakini mwangalie Eliya, yeye alisema, “Nitengenezee mmoja, kwanza. Kwa maana, BWANA ASEMA HIVI, lile pipa halitapunguka na wala ile chupa haitakwisha, hata siku ile Bwana Mungu atakapoleta mvua juu ya nchi.” Hakuna swali, mara akaondoka akaenda kutengeneza mkate na akampa. Kasema, “Nitengenezee wangu kwanza, kisha uende ukajitengenezee wa kwako na mwanao.” Kwa kuwa, yeye alimsikia yule mtu, na akamwangualia; yeye alikuwa mbegu iliyochaguliwa tangu zamani.

⁷⁰ Wengi wao husema, “Yule pale yule maskini mzee mwenda wazimu tena. Mungu anatulaani kwa ajili yake,” kumbukeni, Eliya. Kasema, “Wewe ndiwe mtaabishaji wa Israeli.”

⁷¹ Yeye akasema, “Wewe ndiwe uliyeitaabisha Israeli.” Mnaona ambaye Mungu... Alikuwa akithibitisha Neno la nani? Neno Lake Mwenyewe.

⁷² Sasa Biblia inasema wao waliinuliwa kwa kusudi hili, lakini wakati... a—asiyeamini. Lakini sasa wakati mwamini wa kweli anapoweza kuona Neno la wakati huo limefanyika mwili, Mungu akiongea kupitia midomo ya binadamu halafu anafanya yale hasa Yeye aliyosema angefanya, hilo linatosha!

⁷³ Sasa angalia yaliyosalia. Usiangalie ishara. Kama ukiangalia ishara, utadanganywa kabisa. Manabii wa uongo watainuka na kufanya ishara na maajabu ambayo yatawapoteza walio wateule kama yamkini. Angalieni Neno. Waangalie hawa makuhani, hawa manabii, nabii wa Kiebrania amesimama pale. Zedekia akiwa na pembe mbili kubwa, na akisema, “Mimi ni nabii aliyewekwa wakfu na Mungu.” Ni kweli. “Mimi nina mia

tatu na tisini na tisa wamesimama papa hapa pamoja nami, na Roho Mtakatifu akiwa juu yetu, akithibitisha na kusema ya kwamba ile nchi ni yetu. Hebu twende tukaiteshe. Na kwa pembe hizi, Ahabu, utamfukuza adui atoke nchini mwetu, kwa kuwa Mungu alitupa nchi hii.”

74 Mwangalie huyo mtu wa kidini, mtu mzuri, Yehoshafati, alisema, “Hivi huna mmoja zaidi?”

75 “Mmoja zaidi? Kuna mia nne wanaokubaliana!” Yeye akasema, “Naam, kuna mmoja zaidi hapa, lakini ninamchukia.” Kasema, “Yeye daima anatumbea sisi sote na kutwambia jinsi tulivyo wenye dhambi wakuu, na kila kitu.” Kasema, “Ninamchukia! Yeye, yeye ni Mikaya, mwana wa Imla.”

76 Akasema, “La! mfalme asiseme hivi. Nenda mkamlete na hebu tusikie aliyosema.”

77 Kwa hiyo wakamleta pale. Akasema, “Nipeni usiku wa leo nami nitaona yale Bwana anayosema juu ya jambo hilo.”

78 Ahabu akasema, “Ninakusihii, usiniambie kitu ila kweli.”

79 Ndipo mtu huyo akaja, akasema, “Sasa, kama ukitaka kurudi kwenye ushirika mzuri, sema tu kama wengine wao.”

Mikaya akasema, “Nitasema tu yale Mungu asemayo.” Mnaona?

80 Asubuhi yake, wakatoka. Nao wafalme wakavaa majoho yao, wakaketi kwenye lango, watu wote mashuhuri. Nao wale manabii wamesimama pale, wakasema, “Sasa, ewe mshupavu wa dini, unasemaje juu ya jambo hilo?”

81 Akasema, “Kweeni.” Kasema, “Lakini niliwaona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.”

82 Akampi-. . . akainua mkono wake akampiga mdomoni. Nabii akampiga nabii mdomoni. Sasa, wote wale manabii wawili waliotiwa mafuta wakiwa wamesimama pale, wametabiri, mia nne dhidi ya mmoja, ambao walionekana wana nguvu sana. Sasa, katika wingi wa mashauri si salama kila wakati. Inategemea wao wako wapi. . . wanatoa mashauri juu ya kitu gani, mashauri yao ni nini. Hapakuwepo na usalama pale kwa ajili ya mfalme, naye alichukua wingi wa mashauri yao kuwa ni kweli. Lakini kama yeye angalisimama tu na kufungua gombo na kuangalia yale Eliya aliyokuwa ndio tu amekwisha kusema.

83 Ndipo, Mikaya hakuweza kusema jambo lo lote, yeye hakujua ila labda Mungu alimsamehe jambo hilo. Lakini kwanza, akiwa nabii, yeye alimwendea Mungu apate kujua yale aliyosema Mungu. Ndipo akapata yale aliyosema Mungu. Akasema, “Nalimwona Mungu ameketi katika kiti cha enzi, Naye akasema. . . alikuwa na washauri Wake wote wa Mbinguni wamemzunguka, kasema, ‘Ni nani tunaweza kumfanya ashuke aende akamfanye Ahabu atoke aje huku nje, ili kwamba tupate kutimiza unabii uliotolewa juu yake?’”

84 Mnaona, unabii, Eliya alikuwa tayari alikuwa amesema, “Mbwa watairamba na damu yako.”

85 Na kwa hiyo akasema aliona “pepo wa uongo akipanda kutoka chini, akapanda, akapanda akaja mbele Zake, akasema, ‘Nitashuka nikawaingie manabii wake, manabii wa Ahabu, nitawafanya watabiri uongo.’”

86 Sasa, Mungu alijua ya kwamba watu hao walikuwa wanajigamba sana na wamejaa theolojia mpaka wakafikiri walijua kila kitu. Wao hawakuwa wameliona Neno la wakati huo. Kwa hiyo Mungu akasema, “Utafanikiwa; shuka uende.” Na hapo Mikaya aliposema hayo, hilo liliwafanya kutabiri chini ya pepo mchafu. Wangaling’oa plagi kutoka kwenye simu, ama wangeifunga redio, ama kufanya jambo lo lote; walisikia Hilo likija dhidi yao, wakaamka na kutoka nje. Lakini angalia jambo lililotukia. Sasa, Mikaya ilimbidi kuchunguza ono lake kwa Neno lililoandikwa, kwa hiyo alijua.

87 Akasema, “Nitakapokuja...Mtieni mtu huyo gerezani, mkamnyweshe maji ya shida na kumlisha chakula cha shida. Nitakaporudi, ataniona.”

88 Akasema, “Kama tu ukirudi, Mungu hakusema na mimi.” Hapo ndipo anapojua ono lake linalingana kabisa na kila Neno la wakati huo. Ulikuwa wakati wa Ahabu.

89 Ndugu, dada, hii ndiyo saa na wakati wa kuita kutoka Babeli. Nuru za jioni ziko hapa. Tembea katika Nuru wakati kuna nuru. Angalia, waamini waliona Neno likidhihirishwa nao wanaliamini. Yesu alisema, “Kondoo Wangu wanajua Sauti Yangu, Neno Langu, ishara Zangu za wakati huu. Hawatamfuata aliye wa uongo.”

90 Sasa hebu tuliendee somo letu, maana ninaona nitaliacha. Ninataka kutilia mkazo sana huo mstari wa maombi. Hebu tulirudie lile somo sasa tunalolifikiria, hapa kwa muda kidogo. Vema, litatukia tena kama lilivyofanya daima, kama kawaida.

91 Mungu alimtuma nabii Wake, Yohana, kama Neno Lake lilivyokuwa limesema, lilivyoahidi katika Malaki 3, “Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele Yangu, akaitengeneze njia.” Yohana alishuhudia jambo lile lile. Nasi tunaona pia, katika Isaya 40:3, ya kwamba Isaya alisema, “Kutakuwa na sauti ya nabii, mtu aliaye nyikani, ‘Tengenezeni njia ya Bwana.’” Mnaona? Nabii hizo zote! Halafu—halafu angalieni, angalieni upesi, Maandiko yalimtambulisha.

Wakati wao waliposema, “Wewe u nani? Wewe ni Masihi?”

Akasema, “Mimi siye.”

“Wewe ni Yereimia? Wale manabii, ama mmoja wao?”

92 Akasema, “Mimi siye. Lakini mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, kama alivyosema nabii Isaya.”

⁹³ Unafikiri wao wangeamini jambo hilo? La, bwana. Kwa nini? Yeye hakupitia kanisani mwao. Yeye hakuwa wa ninii yao... Mnaona, alienda jangwani akiwa na umri wa miaka tisa, akatoka akiwa na umri wa miaka thelathini. Ujumbe wake ulikuwa ni muhimu sana asingeweza kupitia kwenye shule ya theolojia; alikuwa ndiye angemjulisha Ma—Masihi. Na kila mtu angekuwa akimvuta *hivi* na *vile*. Naye Mungu alimtuma nyikani, baada ya kifo cha babaye, Zekaria. Naye alikuwa kuhani, bali hakufuata njia ya babaye.

⁹⁴ Maana, manabii hawatoki kwenye vitu vya jinsi hiyo. Wanatoka kwenye nchi za mawe mawe, nyikani. Hakuna mtu ajuaye wanakotoka, ama jinsi wanavyotokea uwanjani, ama yo yote ya historia yao. Wao hutoka tu moja kwa moja na kulihubiri Neno, kisha Mungu anawaondoa, nao hao wanaondoka; wanakihukumu hicho kizazi, na kuingia katika Neno Lake, wakiingojea ile sikukuu.

⁹⁵ Kanisa halikumwamini, kwa maana yeye hakujulikana nao. Wao hawakuwa na kumbukumbu ya kuwekwa kwake wakfu katika vitabu vyao, kwa hiyo basi wao wakamkataa. Mnaona, wao hawakuamini Neno la Mungu lililothibitishwa, wazi, andiko kwa andiko. Mnaona? Malaki 3, Maandiko mawili ya kumthibitisha, Malaki 3 na Isaya 40:3. Mnaona, maandiko yote hayo mawili yalinena habari za kuja kwa mtu fulani, kuitengeneza njia ya Bwana. Alitimiza kila sifa yake.

⁹⁶ Yeye alikuwa awe nabii, “Nitawapelekea Elisha.” Naye alikuwa pale, ni mshupavu kwa kila njia. Angalia jinsi tabia yake ilivyopatana na ile ya Eliya. Eliya alikuwa mtu wa nyikani, na Yohana pia; mtu wa porini. Yeye hakuwa mtu wa mchezo, alikuwa mtu mshupavu.

⁹⁷ Angalia tena, Eliya alikuwa mchukia wanawake, alimwambia Yezebeli juu ya vipodozi vyake vyote, na mahali pa kuingia na kutokea. Na Yohana pia. Yezebeli alijaribu kumwua Eliya, akaapa kwa miungu yake ya kwamba atakikata kichwa chake. Na Herodia pia. Mnaona?

⁹⁸ Daima angalia jumbe zao, angalia yale waliyotenda. Sasa tunaona ya kwamba kama wangaliangalia nyuma na kuona yale Biblia iliyosema, na kuangalia tabia ya mtu huyo na jinsi alivyokubaliana kikamilifu na Maandiko ya saa hiyo na kila kitu, iliwapasa kujua ya kwamba huyo alikuwa ndiye. Karibu nusu dazani walijua jambo hilo. Hiyo ni kweli. Si zaidi ya nusu dazani waliotambua jambo hilo. Walienda kumsikia, bali hawakuamini jambo Hilo. Mnaona? Kwa nini? Wao hawakuamini kutambulishwa kwa unabii katika saa yao.

⁹⁹ Angalia, walimcheka, wakimwita “mtu mwitu fulani, mshupavu wa dini anayepiga makelele, asiye na elimu wala kisomo, ‘ii, siho, iyo, pepa, dafuta,’ na kadhalika.” Kama kawaida wao wanampima kwa elimu yake. Wanampima kwa

sarufi yake, namna alivyovalia. Yeye alijifunga kipande cha ngozi ya kondoo, na kuvaa mshipi wa ngozi ya ngamia, alikuwa mwenye nywele nyingi. Akitoka kwenda majini; hana kanisa, hana kiti cha kikuhani, hana mtu anayeshirikiana naye; wao hawakuweza kukubali jambo hilo; walikuwa wakimwabudu mungu wa dunia. Mnaona?

¹⁰⁰ Simaanishi kusema sasa hakuna manabii wa uongo wanaotokea, kama akina Yane na Yambre. Lakini jinsi ambavyo ungepaswa kufanya, ni kuchunguza ujumbe wa asili kwa Neno, ndipo umelipata jambo hilo; liko kwenye wakati gani, na ni kitu gani kilichotabiriwa kwa ajili ya huo wakati.

¹⁰¹ Basi unabii wa Yohana ulidhihirishwa katika utaratibu wa Mungu Mwenyewe. Angalia jinsi lilivyo kamilifu. Biblia ilisema, “Neno la Mungu linamjia nabii.” Naye Yesu alikuwa Neno. Na Yohana alikuwa akitabiri juu ya kuja kutimizwa kwa Neno; na Yesu, Neno, akaja kwa nabii, majini. Loo, linapendeza jinsi gani! Jinsi ninii lisivyoshindwa . . . Mnaona? Neno lilikuwa haba katika siku hiyo. Huyu hapa yuaja nabii, akisema, “Mimi ni sauti ya Neno.”

Wao wakasema, “Tufanye nini?”

¹⁰² Kasema, “Mimi sistahili kufungua viatu vyake. Lakini kuna Mmoja anayesimama kati yenu, mahali fulani, atakuwa Ndiye atakayewabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto. Pepeto Lake li mkononi Mwake, Naye atausafisha sana uwanda Wake, na kuyateketeza makapi kwa moto usiozimika, atakusanya ngano ghalani.” Loo, ni nabii wa namna gani! Yesu alisema hapakutokea mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama yeye, mpaka siku hiyo. Loo, jinsi anavyojiamini! Jinsi alivyojua amesimama wapi! Yeye alijua kwa hakika kabisa. Alikwisha sikia kutoka kwa Mungu, na ilikuwa inalingana kabisa na Neno, kwa hiyo hakujali watu wanasema nini. Yeye alililhubiri na kulitabiti, hata hivyo. Na uangalie, mtu anaposimama kwa yaliyo Kweli, basi Mungu anawajibika kumdhahirishia huyo mtu ile kweli.

¹⁰³ Wakati Musa alipoenda zake Misri, na kusema, “Nilikuwa huko jangwani, nami nikaona mti unawaka moto, wala haukuungua. Nikauendea ule mti, na, nilipofanya hivyo, kulikuwa na Nguzo kubwa ya Moto hapo ndani inaning’inia. Na Sauti ikasema, ‘MIMI NIKO AMBAYE NIKO.’ Naye ameniambia nichukue fimbo hii na kushuka nije hapa na kufanya miujiza hii, Naye Mungu atalithibitisha Neno Lake.” Akainyosha fimbo yake, kukatokea viroboto na inzi, na giza na kadhalika. Halafu ili kumthibitisha huyo nabii, Yeye aliwaleta hao waamini moja kwa moja kwenye ule mlima, Naye Mungu akashuka chini katika Nguzo ile ile ya Moto, juu ya mlima ule ule, na kuthibitisha ya kwamba hiyo ilikuwa ni kweli.

Sasa angalieni alichofanya katika siku hii. Namna ile ile.

¹⁰⁴ Sasa, Neno likamjia nabii na kumthibitisha kwamba yeye ndiye mtu sahihi, ndiye hasa mtu ambaye Maandiko yalisema angekuwa ndiye. Upesi sasa. Lakini, tena, Yesu alikuja katika namna tofauti mbali na fasiri yao ya unabii. Mwanadamu alikuwa amefasiri mambo yangeendaje. Ndiyo. Wapresbiteri wanafikiria inapaswa kuwa ni wao. Angalia wakati Mungu anapofanya jambo lo lote, angalia kila madhehebu mengine yanapoinuka na moja na. Naam, daima imekuwa namna hiyo. Wao wana Yane na Yambre kila mahali. Angalia, walina sehemu ya Neno. Lakini, kulingana na Neno la nabii, kila Andiko!

¹⁰⁵ Walishindwa kuliona, kama kawaida, wakamwita mpiga ramli, “pepo; Belzebuli,” na wakasema Yeye alijifanya Mwenyewe Mungu, wakati iliwapasa kujua, kwa Biblia yao wenyewe kabisa, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu.

Angalia, Yeye alitabiriwa na Isaya, Isaya 9:6, ilisema, “Jina Lake ataitwa Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele.” Hakutakuwako na baba wengine baadaye, maana Yeye alikuwa ndiye Baba wa kwanza hapo mwanzo, Yeye ndiye Baba pekee; kasema, “Wala msimwite mtu ye yote wa dunia hii ‘Baba,’” wala, baada ya hapo.” “Yeye ni—ni Mungu Mwenye Nguvu, na Baba wa Milele, Mshauri, Mfalme wa Amani.” Bila shaka.

¹⁰⁶ Sasa, wao walikuwa wamemtendea yale manabii wote waliyosema ya kwamba wangefanya, kama tu wanavyofanya katika Wakati huu huu wa Laodikia, kumtupa Yeye nje ya kanisa. “Vipofu, uchi, na hawajui.” Kama tu alivyosema nabii, nabii wa Biblia. Walipofushwa na mapokeo ya mwanadamu, wakamtupa nje, Neno wakalitupa nje ya makanisa yao, kama kawaida, kama walivyotabiriwa.

¹⁰⁷ Angalieni sasa, upesi sasa. Msikose jambo hili sasa. Hili hapa somo, jinsi Yesu alivyojitambulisha Mwenyewe kwa wanafunzi hawa wawili ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi wao! Sasa, macho yote yatazame huk. Na nje huko nchini, msipitwe na jambo hili sasa. Tumejaribu kuwaambieni ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu, lililoandikwa na Mungu Mwenyewe, kwa midomo na kwa njia ya mwanadamu. Mungu anaweza kuandika, Yeye Mwenyewe. Mungu anaweza kuongea, Yeye Mwenyewe. Mungu anaweza kufanya atakalo, lakini alimchagua mwanadamu kufanya hivyo kwa sababu mtu aliyeliandika Hilo ni sehemu ya Mungu. Kwa hiyo, Mungu ndiye aliyeliandika Biblia. Hao watu hata hawakujua walichokuwa wanaandika, katika kuwaza kwao kwa kibinadamu. Huenda wasikubaliane nalo, lakini waliliandika jambo hilo. Wasingeweza. Biblia ilisema, “Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu!” Mungu aliongoza mikono yao, akaongoza macho yao katika maono. Wao hawakuweza kusema kitu cho chote ila kile walichokuwa wanaangalia. Hawangeweza kunena kitu, maana Yeye alitawala kabisa ulimi, kidole, kila kiungo cha mwili

kilikuwa katika utawala mkamilifu wa Mungu. Si ajabu Biblia ilisema wao walikuwa miungu, walikuwa ni sehemu ya Mungu! Yeye alikuwa Ndiye utimilifu wa Mungu.

¹⁰⁸ Angalia jinsi Yesu, lile Neno, alivyowafanya hawa wanafunzi wawili waliovunjika moyo kujua Yeye alikuwa ndiye Masihi wao, Masihi, Neno lile lililoahidiwa. Angalia alilofanya, Yeye alirejea kwenye unabii. Angalia, “Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoandika manabii.” Sasa, Yeye hakusema kamwe, “Vema, kanisa linasema nini kuhusu, kuhusu jambo hilo?”

¹⁰⁹ Wakamsimulia hicho kisa. Walijua matukio yote yaliyotukia. Walikuwa na huzuni sana. Wakaanza kumwambia Yeye, “Je! Wewe peke yako u mgeni hapa, ama Wewe huyajui yaliyotukia kule Yerusalemu?”

¹¹⁰ Akasema, “Mambo gani?” kana kwamba Yeye hakujua. Mnaona, Yeye hufanya mambo wakati mwingine ili tu aone yale utakayofanya juu ya jambo hilo. Mnaona? Kasema, “Mambo gani? Alikuwa ni nani? Kitu gani kimetukia?”

¹¹¹ “Je! Wewe peke yako u mgeni?” Nao walikuwa wanazungumza moja kwa moja na Mtu waliyekuwa wameishi naye kwa miaka mitatu na nusu, nao hawakumjua Yeye.

“Mambo gani? Nini kilichotukia?”

¹¹² Vema, wao wakasema, “Yesu wa Nazareti, ambaye alikuwa Nabii. Hakuna shaka mioyoni mwetu. Yeye alikuwa hodari katika Neno na katika matendo mbele za watu wote. Tulimwona akifanya mambo yaliyomtambulisha kama nabii wa Mungu kwa ajili ya wakati huu. Tunajua jambo hilo. Nasi tuliamini ya kwamba Yeye ndiye angekuwa Mkombozi, ya kwamba Yeye angemkomboa Israeli.”

¹¹³ Ndipo anageuka na kusema, “Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kufahamu ya kwamba yote waliyosema manabii juu Yake hayatatimia?” Mnaona? Mwangalie Yeye sasa akirudi kwenye unabii. Ni kemeo la jinsi gani kwa waamini, walidai walimwamini!

¹¹⁴ Angalia jinsi alivyoliendea somo hilo. Yeye hakuja moja kwa moja na kusema, “Mimi ni Masihi wenu.” Angeweza kufanya hivyo, kwa kuwa ndivyo alivyokuwa. Lakini angalia Yeye alijitambulisha Mwenyewe katika Neno, ndipo wao wangejua. Kama Yeye angalisema jambo hilo, angalisema jambo hilo wala lisingekuwa ni kweli; bali alipoenda na kuanza kunena juu ya yote yale manabii wote waliyonena juu Yake, nao wakaona jambo hilo, basi waliweza kujua wao wenyewe, kama wao walikuwa watoto wa Mungu. Bali aliwaelekeza kwenye yale waliyokuwa wametabiri manabii na kusema yatazamiwe katika wakati ambao Masihi, wakati Wake ungedhihirishwa. Yeye, kama vile Yohana, aliacha Neno, Biblia iutambulishe Ujumbe wao. Nabii ye yote wa kweli angefanya jambo hilo. Hakutoka

na kusema, “Mimi Ndiye. Ndimi. . .” Huyo si nabii wa kweli wa Mungu. Mnaona? Lakini Yeye alisema, “Rudini kwenye Maandiko.” Mnaona, Yeye hashindwi kwenye njia Yake ya kufanya jambo hilo. Mnaona?

Akasema, “Tunamjua Musa.”

¹¹⁵ Akasema, “Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi.” Akasema, “Musa aliandika habari Zangu.” Kasema, “Yachunguzeni Maandiko, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, nayo Maandiko ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Nendeni mkayachunguze Maandiko na mwone jambo hilo.”

¹¹⁶ Hapa Yeye habadilishi kamwe njia Yake ya kufanya jambo hilo, hajabadilisha hata kidogo. Hawezi kamwe kubadilika, kwa maana Yeye ni Mungu asiyebadilika. Mnaona? Angalia alirudi moja kwa moja kwa hawa wanafunzi wawili, Kleopa na rafiki yake, wakienda zao Emau, na kusema, akawarjeshia kwenye Maandiko, akasema, “Kwa nini ninyi ni wajinga sana kutoamini kwamba kila Neno waliloandika manabii kumhusu Masihi lingebidi kutimizwa?” Loo, ni siku ya namna gani!

¹¹⁷ Yohana alifanya jambo lile lile. “Chunguzeni Maandiko, angalieni nyuma, yalisema kungekuweko na ‘sauti ya mtu aliaye nyikani.’ Je! Mimi nilitoka wapi?” Mnaona? Hilo, hilo lingalipaswa kulifanya jambo hilo dhahiri kwao. Kweli!

¹¹⁸ Lingepaswa kulifanya dhahiri leo, jambo tunalomwona Roho Mtakatifu akifanya. Yeye alisema wakati mmoja, “Chunguzeni Maandiko.” Nasi. . . Yeye anatutaka kufanya jambo hilo leo.

¹¹⁹ Angalia, Yeye alianza na unabii wa Musa, Biblia ilisema, “Yeye, akianza kutoka Musa na manabii wote,” lakini alianza na Musa. “Nabii,” alisema Musa, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea kati yenu enyi watu, kati ya watu. Bwana Mungu atawaondokeshea Nabii.”

¹²⁰ Sasa huenda alikuwa amesema, “Kleopa, na rafiki yako hapa, je! Musa hakusema ya kwamba katika siku hizi Bwana Mungu angewaondokeshea Nabii? Na Mtu huyu waliyemsulubisha, je! Yeye alitimiza sifa hiyo? Sasa, Musa alitabiri jambo hili. Na sasa ninyi hamjawa na nabii kwa mamia na mamia ya miaka, na hapa Mtu huyu amefufuka. Na mtangulizi wa Mtu huyu alikuwa nani, Yeye alisemaje?” Mnalipata? Na yote yale waliyosema manabii juu Yake, kwa ajili ya wakati Wake, Yeye alinena nao. Hakika wanalifurahia kumsikiliza. Je! wewe usingalipenda kumsikiliza? Laiti ningalimsikiliza, kumsikia, yale aliyosema ya kwamba manabii walinena juu ya nafsi Yake Mwenyewe, bali Yeye hakusema alikuwa Ndiye. Yeye aliwaonyesha tu kwa unabii. Alisema tu, “Nabii alisema jambo hili lingetukia.” Mnaona?

¹²¹ Hebu na turudi tu nyuma dakika chache, na sasa hebu tusikilize Maneno yaliyonukuliwa kutoka Kwake Mwenyewe.

Angalieni hapa, Neno Lenyewe likinukuu Neno Lake Mwenyewe. Neno Lenyewe likinukuu Neno Lake Mwenyewe. Si kuwaambia ya kwamba alikuwa hivyo, lakini kuachilia tu Neno lijinee Lenyewe, ndipo wanajua Yeye alikuwa ni Nani. Andiko la Neno, likinukuu Neno katika . . . Neno katika mwili, likinukuu Neno la andiko, likiwa limetambulishwa kikamilifu Naye Mwenyewe. Angalia hapa, sasa hebu tumsikilize Yeye akinukuu. Jinsi sasa tunajua ya kwamba wote walipashwa habari kwa kifupi juu ya matukio ya juzijuzi, yaani, kuhusu kusulubishwa pamoja na habari za kufufuka, lile kaburi, kama tulivyosoma hivi punde. Sasa Yeye anaenda moja kwa moja kwenye Neno la unabii kumhusu Yeye Mwenyewe. Sasa hebu tu tufikirie ya kwamba Yeye alisema hivi; Yeye alisema mengi zaidi ya haya, lakini angalieni.

¹²² Hebu tuseme Yeye . . . tumsikie Yeye akisema, “Fungueni Zekaria 11:12. Je! Masihi si alikuwa auzwe, kulingana na nabii, kwa vipande thelathini vya fedha? Mmesema hivi punde tu ya kwamba Mtu huyu aliuzwa kwa vipande thelathini vya fedha.” Fungueni. Mnayapata hayo Maandiko? Zekaria 11:12. Na halafu Yeye akasema, “Je! mlitambua yale Daudi aliyosema katika Zaburi, Zaburi 41:9? Yeye alikuwa asalitiwe na rafiki zake. Na halafu tena, katika Zekaria 13:7, Yeye aliachwa na wanafunzi Wake. Na katika Zaburi 35:11, alishtakiwa na mashahidi wa uongo. Sasa hivi tu mmesema alishtakiwa. Isaya 53:7, Yeye alifunga kinywa Chake mbele ya washtaki Wake. Isaya 50:6, walimpiga mijeledi, ndivyo alivyosema nabii. Zaburi 22, ilikuwa alie msalabani, ‘Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?’ Je! Yeye alifanya hivyo, juzi alasiri? Zaburi 22 tena, 18, nguo Zake ziligawanywa miongoni mwao. Je! wao walifanya jambo hilo? Na Zaburi 22:7 hadi 8 alidhihakiwa na adui Zake, kanisa. Zaburi 22 tena, hapakuwepo na mfupa mwilini Mwake utakaovunjwa, lakini ‘walinizua mikono na miguu,’” Yeye alisema. Akishikilia mikono Yake nyuma Yake, hapana shaka, wakati huo. “Isaya 53:12 ilisema Yeye angekufa katikati ya wahalifu. Isaya 53:9 ilisema alizikwa pamoja na matajiri. Zaburi 16:10 ilisema, ‘Sitaiacha nafsi yake kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu.’ Na je! Malaki 3 haikuwa mtangulizi wa Mtu huyu?” Loo, ningalipenda kumsikia akinukuu hayo. Angalia zile nabii! Angalia, halafu mifano yote ambayo angaliipitia, kuhusu Isaka, katika Mwanzo 22, jinsi Mungu alivyomwonyesha Isaka katika kivuli, jinsi baba Ibrahimu alivyomchukua mwanawe mwenyewe, anapanda kilima huku amebeba kuni, na akamtoa mwanawe.

¹²³ Sasa lilikuwa likianza kuwaelea. Yeye tayari alikuwa amewaambia walikuwa wajinga kwa kutoangalia unabii wa siku hiyo. Na sasa likaanza kuwaelea, wakaanza kuona kutimizwa kwa yote haya yaliyokuwa yametukia katika siku chache zilizopita, katika miaka miwili ama mitatu iliyopita, unabii

uliohibitishwa wa wakati huo. Hapo ndipo ambapo walijua ya kwamba rafiki yao aliyesubishwa, Yesu, alikuwa ametimiza kila Neno la mambo haya. Loo! hapo ndipo ambapo walijua ya kwamba Mtu huyo alikuwa ndiye Masihi yule, ya kwamba—ya kwamba alipaswa kufufuka katika wafu. “Kaburi lisingemzuia. ‘Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu.’ Hakuna daima hata Neno moja la unabii linaloweza kushindwa. Naye kweli alifufuka.”

¹²⁴ “Basi hao wajumbe pale kaburini asubuhi ya leo walisema kweli. Yeye amefufuka katika wafu. Yu hai. Yeye Ndiye yule Masihi.” Kwa nini? [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu] Msipitwe na jambo hilo. “Kutenda Kwake, huduma Yake na kila kitu alichofanya kimethibitisha sawasawa kabisa Maneno ambayo nabii alisema yatatukia kwenye siku hii. Hilo lilitosha.” Ndipo walipojua ya kwamba alikuwa Ndiye, rafiki yao aliyesubishwa, Yesu, ambaye alikuwa amefanya jambo hilo. Si ajabu mioyo yao iliwaka ndani yao hapo alipokuwa akisema nao. Sasa wao walikuwa wametembea maili sita, na ilionekana kama muda mfupi.

¹²⁵ Na hapa kuna jambo lingine walilofanya, mwajua, tayari wamesikia ujumbe wa masaa sita juu ya unabii ukithibitishwa. Hayo ndiyo alinena nao njiani. Mara tu walipoanza kwenda njiani, Yeye akatokea, kwa maana alikuwa pale pale Yerusalemu. Masaa sita ba-a-...baadaye, vipimo sitini, walikuwa njiani wakienda zao maili sita kuelekea Emau. Hivyo ndivyo ilivyo. Naye alikuwa amehubiri, akathibitisha unabii kwa masaa sita. Msinilaumu kwa yangu matatu, basi, mnaona. Mnaona? Lakini angalieni, walikuwa wamehubiri... Yeye...Walikwisha sikia ujumbe wa masaa sita juu ya unabii ukihakikishwa, kuthibitishwa.

¹²⁶ Sasa ilikuwa inaelekea wakati wa jioni. Mwajua, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hapo ndipo alipoyafungua macho yao kujua ya kwamba Waebrania 13:8, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Wakati wa jioni, matukio yanadhihirishwa na unabii. Yale yanayotukia katika wakati huu yanaweza kutambulishwa kwa urahisi kama mtaamini tu unabii wa wakati huu.

¹²⁷ “Naam, enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito kufahamu, wenye mioyo mizito kuamini (mnaendelea kuwazia jambo hilo,) kuamini ya kwamba yote waliosema manabii juu ya Masihi, je! si ingebidi yatukie?” Sasa Yeye alichunguza mambo haya yote muhimu huko nyuma kote na kuonyesha yale nabii aliyosema kwamba yangetukia. Ndipo wakaanza kufahamu. Kwa hiyo Yeye alisema...alifanya kana kwamba anaendelea mbele. Wao walimpenda Mtu huyu. Wakasema, “Wewe, Wewe umetupa kitu fulani. Hatukuwazia juu ya hayo. Yeye yu hai mahali fulani.” Walikuwa wanazungumza Naye, hawakujua jambo hilo. Kwa hiyo Yeye...na hapana shaka aliwaangalia kwa huzuni, na akaanza kupita, lakini Yeye—Yeye alikuwa

akingojea wamkaribishe. Hilo ndilo analongojea usiku wa leo, wewe kumkaribisha.

¹²⁸ Basi angalia wakati hao wanafunzi walipomkaribisha katika ushirika wao mezani, hapo ndipo ambapo alitenda jambo fulani kama vile tu alivyofanya kabla ya kusulubishwa Kwake, ndipo macho yao yakafunguka. Walijua tabia Yake, mtindo Wake. Walijua alichofanya, Naye alifanya jambo hilo kama tu alivyofanya hapo zamani. Nao wakasema, “Huyo Ndiye!” Na upesi wakasimama wapige mayowe, Naye akatoweka. Na mahali ambapo walichukua masaa sita kusikiliza mahubiri haya, labda walitumia dakika ishirini kukimbia kurudi kuwaambia wale wengine, “Amefufuka kweli. Yeye kweli yu hai.”

¹²⁹ Marafiki, hii ni kutimizwa kwa Malaki 4, Luka Mtakatifu 17, Yohana Mtakatifu 15, loo, mengi sana, Ufunuo 10, nabii nyingi sana zinazoweza kutambulishwa kabisa kwenye siku hii. Na pia katika Kitabu cha Marko na katika Mathayo, ambapo Yeye alisema ishara hizi kuu na maajabu yangetokea mbinguni, nao watu wanasema ni visahani, visahani virukavyo, vi—vinaweza kutoweka kwa nguvu na wepesi wa wazo, viumbe vinavyoweza kunyemelea. Yeye anaweza kuandika, Yeye anaweza kuongea, Yeye anaweza kufanya lo lote atakalo. Ile Nguzo kuu ya Moto, “yeye yule jana, leo, na hata milele.” Na mambo makuu yakija juu ya dunia, piramidi za moshi zikipanda hewani, huko juu kabisa mbali na mahali ambapo hapawezi kuwa na unyevu wala kitu cho chote, maili thelathini kwenda juu. Lilitabiriwa mwaka mmoja na nusu kabla halijatukia, ya kwamba lingekuwa namna hiyo. Halafu ugeuze picha uone ni Nani anayetazama chini. Hakuna hata Neno moja ambalo limenenwa limewahi kushindwa, na hili hapa Neno la Mungu lililoandikwa, likithibitisha kwamba ni Kweli. Na ni wakati wa jioni tena. Sijui kama Yeye angerudi, kwa neema, usiku wa leo na kufanya jambo fulani sasa kama alivyofanya huko nyuma. Hebu tuombe na kumwuliza Yeye. Matukio yakithibitishwa na unabii uliothibitishwa.

¹³⁰ Mungu Mwenyezi, tusaidie. Tusaidie Mungu Mpenzi, kufahamu, kufahamu mambo ambayo tunapaswa kujua, kufahamu Neno Lako. Na sasa, Bwana, tumesikia mahubiri sasa kwa karibu miaka elfu mbili, maandishi ya vitabu. Na katika siku hizi za mwisho hapa jambo hilo limejipenyeza moja kwa moja tena, na sasa inaelekea wakati wa jioni. Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, na wengi wao katika wakati wote huu uliopita wamezungumza pamoja na Wewe, na labda mahali fulani tu njiani kwenye siku hii kuu ambayo haijakuwa aidha mchana wala usiku, kama nabii alivyosema, lakini katika wakati wa jioni kutakuwako Nuru. Yesu alifufuka kutoka kaburini na kumtokea Simoni na hao wanawake, na akawaonyesha ya kwamba alikuwa hai. Hiyo ilikuwa ni asubuhi. Halafu jioni akarudi tena. Lakini aliwatembelea mchana kutwa, akiwakemea

kwa upofu wao, lakini badaye akajitambulisha Mwenyewe kwao wakati wa jioni.

¹³¹ Mungu, njoo kwenye ushirika wetu usiku wa leo tulio nao kwenye Neno. Mungu, ni jambo linaloaminiwa kwa shida sana miongoni mwa watu leo, lakini ninashukuru ya kwamba kuna wengine ambao Wewe umewaita na kuwachagua kwa ajili ya Uzima wa Milele, Nawe ulisema, “Wote alionipa Baba watakuja.” Na sasa wakati Nuru za jioni zinapoangaza, wakati Wewe umeruhusu, Bwana, ya kwamba hakuna hata unabii mmoja (kutoka kwa mamia ambayo yametolewa) umekosea hata wakati mmoja. Basi kama kweli huo ukijitambulisha, haina budi kuwa ni Wewe, maana hakuna mtu anayeweza kuwa sahihi namna hiyo. Kama tu vile Biblia, hakuna mtu angaliweza kuandika, hakuna mtu katika muda wa mika elfu moja mia sita, ikiandikwa na waandishi arobaini tofauti, wangeweza kuandika, na kusiwe na hata kosa moja ndani yake.

Mungu mpendwa, ninaomba ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe usiku huu, kwa Waebrania 13:8, ya kwamba ni Wewe yule jana, leo, na hata milele. Na kazi ambazo ulifanya wakati huo, Wewe unazifanya leo. Nawe uliahidi jambo hilo, ulisema, “Katika siku hizi za mwisho, wakati ulimwengu uko kama Sodom na Gomora, upotovu.” Tunawaangalia hawa vijana wanaofanana sana tu na wasichana, wakivaa nguo kama wao, na—na kuona wasichana wakijaribu kuwa kama wavulana, na kuwaona wanawake na wanaume katika wakati huu uliopotoka, kuona kwamba tamaa ya kujuana kimwili imekuwa sa—sanamu ya kuabudu. Injili imesukumwa kando, na utupu katika banisa la Laodikia. Ee Mungu, ni majira ya namna gani! Njoo, Bwana Yesu, jijulishe kwetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu.

¹³² Sasa wakati vichwa vyenu vimeinamishwa, macho yenu yamefumbwa, nitawaulizeni jambo fulani. Je! mnaamini ya kwamba Mungu yuko hapa? Je! mnaamini ya kwamba mambo ambayo Hilo linatenda leo ni unabii ukitimizwa? Mnaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnaamini wakati alipokuwa hapa na akadhihirishwa katika mwili kwa ajili ya siku hiyo, na kazi alizofanya kule, zingerudiwa tena siku hii? Nabii alisema hivyo. Biblia ilisema hivyo. Maandiko yote hayana budi kutimizwa, hayawezi kushindwa. Yeye alijitambulisha namna gani? Kwa kuwa yule nabii ambaye Musa alinena habari zake. Alijua siri za mioyo ya watu. Yule mwanamke aligusa vazi Lake, akageuka akasema, “Imani yako imekuokoa.” Wakati Simoni Petro alipomjia, Yeye alijua jina lake, akamwambia alikuwa nani, baba yake alikuwa nani. Na Yesu yuyo huyo mwema hajafa, Yeye yu hai milele. Mungu asifiwe! Nami ninaamini, katika wakati huu wa jioni sasa, Yeye ametuita pamoja tena.

¹³³ Ee Bwana Yesu, njoo miongoni mwetu. Usitupite. Njoo, ukae nasi usiku kucha mpaka usiku huu utakapokwisha, kisha

uturuhusu kwenda pamoja Nawe kesho, kusudi tupate kukujua Wewe katika nguvu za kufufuka Kwako, ili kwamba upendo Wako na neema na rehema zipate kuwa pamoja nasi. Ee Mungu wa Milele, tujalie mambo haya. Tunajua ya kwamba Mungu peke Yake ndiye anayeweza kutupa hayo.

¹³⁴ Katika uchaji wa saa hii, hebu tusema jambo hili: Mungu, Baba yetu, miili yetu ni maskani mbovu kwa ajili Yako. Lakini, Bwana, hebu neema Yako itakasayo, Roho Wako Mtakatifu, aje sasa. Tusafishe na kila shaka na kila hangaiko, na kila shuku na kila njia ya kutilia shaka ambayo ingekuwa ndani yetu, ili tupate kuwa huru bila shaka hata moja; njoni, mkiri kwa ujasiri kama Petro, “Wewe Ndiwe Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹³⁵ Tunaamini ya kwamba Neno Lako ni Kweli, Bwana. Hebu tuone tu kabla hatujaanza mstari huu wa maombi, Bwana, Nawe ujijulishe kwetu. Kama vile Wewe ulivyosema, “kama ilivyokuwa katika siku za Lutu,” wakati Ibrahimu, hilo kundi lililoitwa linamngojea mwana wa ahadi. Lutu alikuwa kule chini akimsikiliza Billy Graham wa kisasa na Oral Roberts kwenye ule mpango wa kimadhehebu kule, kama taifa. Lakini Ibrahimu alikuwa mgeni bila madhehebu yo yote, kundi hili dogo tu lililokuwa linatangatanga kila mahali katika nchi ambayo alikuwa arithi. “Na walio wapole watairithi nchi.” Siku moja, chini ya mti wenye kivuli, walipokuwa wameketi, wamepumzika, Mungu alishuka katika mfano wa Mwanadamu. Malaika wawili walishuka wakaingia Sodoma. Naye Mungu, katika mwili wa kibinadamu, alithibitisha ya kwamba alikuwa Ndiye, akasema, “Ibrahimu, yu wapi mke wako, Sara?” Siku chache kabla ya jambo hilo, yeye alikuwa Abram; naye S-a-r-a-i, Sarai; si Sara, “binti mfalme.” Nawe ulimwita kwa jina lake la kifalme, binti wa mfalme. Ulimwita Ibrahimu kwa jina lake, Ibrahimu, baba wa mataifa. Nawe ulisema, “Nitakurudia.”

¹³⁶ Mungu, jinsi gani ilibidi moyo wa nabii yule kuruka! Yeye alijua Wewe ulikuwa ni Nani papo hapo. Si ajabu yeye alikuosha miguu Yako, akatoa chakula chote alichokuwa nacho, na kilicho kizuri sana, akakiweka mbele Zako. Yeye alijua huyo hapo alikuwa ni Mungu. Ndipo akasema, “Yu wapi Sara?” kana kwamba Yeye hakujua. Nawe . . .

¹³⁷ Ibrahimu akamwambia, “Yeye yumo hemani . . . yumo hemani, nyuma Yako.”

¹³⁸ Nawe ulisema mambo yatakayotukia. Naye, moyoni mwake, alitilia shaka jambo Hilo. Na ndipo Wewe—Wewe ukamwambia Ibrahimu, “Kwa nini Sara alitilia shaka jambo hilo, akisema moyoni mwake, ‘Mambo haya hayawezekani?’ Kuna neno lililo gumu la kumshinda Mungu?”

¹³⁹ Ee Mungu! Yesu, Mungu aliyedhihirishwa wa Neno, ulisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” ulimwengu ungekuwa katika hali hiyo kabla tu ya kuangamizwa kwa

ulimwengu wa Mataifa, Majira ya Mataifa. Tumewasili, Wasodoma kweli kweli! Halafu ulisema ya kwamba Mwana wa Adamu, ambaye daima anaitwa “nabii,” angefunuliwa katika hiyo saa. Timiza Maneno Yako, Ee Mungu. Sisi, watoto Wako wanaoamini, tunangojea tukiwa na mioyo miaminifu, utupe imani, Bwana. Ili kwamba, tutakapofanya mstari wa maombi, watu wataamini. Ni wakati wa jioni, Baba. Naomba Nuru za jioni za Mwana wa Mungu (Yeye Aliyekuwako, na Yeye Aliyeko, na Atakayekuja) ajidhihirishe Mwenyewe kwa unabii ambao ametoa. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁴⁰ Sasa niko tayari ku—kuwaombea wagonjwa. Lakini ni jambo la ajabu jinsi ambavyo wakati tunaposimama hapa, na hapa nasimama hapa sasa nikitoa sai kwa hadhara, na tumeunganishwa kwa simu kila mahali nchini, ya kwamba Mungu angali ni Mungu. Yeye hawezi kushindwa. Na yale anayoahidi, hayo atafanya. Yeye hatashindwa kamwe kufanya jambo hilo, kwa maana Yeye aliahidi kufanya hayo. Kwa hiyo ninaweza kuweka imani yenye uchaji katika yale aliyosema. Kwa hiyo ninakutazamia Kuja Kwake, ninamtazamia kutokea wakati wo wote, kwa maana alisema, “Katika saa msiyodhanja,” isiyodhaniwa na ulimwengu, “ndipo Yeye atakapotokea.”

¹⁴¹ Sasa, kadiri ni juavyo mimi. . . Niko kwenye Maskani yangu hapa, na kuna watu wachache wanaoketi hapa ambao ni—ninawajua. Ndugu Wright, wachache wa hawa wanaoketi hapa, ambao papa hapa, ninawajua. Lakini kuna wengi wenu siwajui. Nami sina njia ya kusema ya kwamba Mungu atafanya jambo hili usiku wa leo. Tumemwona akitenda jambo hilo kwa miaka kadha wa kadha iliyopita, lakini huenda asilifanye usiku wa leo. Sijui. Hiyo ni juu Yake. Yeye ni mwenye enzi. Yeye hufanya atakayo. Hakuna mtu anayeweza kumwambia la kufanya. Yeye hudumu peke Yake, katika mapenzi Yake na njia Zake. Lakini kwa sababu Yeye aliahidi jambo hilo, ninamwomba alifanye. Si kwa ajili yetu, kwamba tunahitaji jambo hilo, bali kwa ajili ya baadhi ya wageni, kusudi Roho Mtakatifu atiwe upako. . . Sasa Yeye. . . apate kututia upako. Sasa, haidhuru Yeye anitie upako namna gani, hana budi kuwatia upako, pia, bila shaka, mpate kuamini.

¹⁴² Sasa ninataka kufanya mstari wa maombi, nami ninataka kuwaombea wagonjwa wengi kadiri niwezavyo. Sasa, aidha tunaweza kufanya mstari, kuwaita watu na kuwaleta hapa, mstarini wa maombi na kumwombea kila mtu hapa aliye mgonjwa, nadhani, niwalete ndugu zangu wahudumu waje hapa tuwe pamoja, na kuwawekeeni ninyi mikono. Hakika tunaweza kufanya jambo hilo. Ama aidha tunaweza kumwomba Baba yetu, Ambaye Ndiye tu angeweza kuwafanyia jambo lo lote, kwa maana mikono yangu ni kama yako ewe mtu. Lakini jambo lenyewe ni kwamba, si mkono wa mwanadamu unaofanya jambo hilo; ni Neno la Mungu. Imani katika hilo Neno ndiyo

inayotekeleza jambo hilo. Hakuna jambo la kisayansi juu yake, si la kisayansi kabisa.

¹⁴³ Hakuna kitu hata kimoja alichu nacho Mkristo katika silaha zake ambacho ni cha kisayansi. Je! mlijua jambo hilo? Upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, upole, utu wema, saburi, imani, Roho Mtakatifu, kila kitu ni kisichoonekana na sayansi. Na hicho ndicho kitu pekee kilicho halisi na kidumucho. Kila kitu unachoangalia hutokana na dunia na kinarudi duniani. Lakini vitu usivyoweza kuona kwa jicho lako, lakini unakiona kikijitangaza Chenyewe, huo ni ulimwengu wa mambo ya Milele.

¹⁴⁴ Ungeweza kuamini, kama Mungu angeweza kujidhihirisha Mwenyewe na kuonyesha ya kwamba Yeye yu hai hapa, akifanya mambo yale yale aliyofanya hapo mwanzo, baada ya Ujumbe huu, ungekubali jambo hilo kama kuponywa kwako? Mungu na atujalie. Sasa naomba kila mtu katika nyumba hii, haidhuru wewe ni nani ama umetoka wapi, ninakusihi uamini tu kwa uchaji Ujumbe huu kuwa ni Kweli. Huo ndio Ujumbe alio nao Mungu katika Biblia Yake kwa ajili ya saa hii, ya kwamba Yesu Kristo yuko hapa usiku wa leo na yu hai. Sasa karibuni . . .

¹⁴⁵ Ninyi watu wote mnanijua mimi, niko papa hapa mjini nilipolelewa. Hata sina elimu ya msingi. Hiyo ni kweli kabisa. Nanyi mmenijua muda mrefu vya kutosha, natumaini nimeishi mbele zenu kuwaonyesha ya kwamba mimi ni mkweli na ni mwaminifu. Mimi si mnafiki. Hata wapinzani wangu hawasemi hivyo. Wao, wao wanasema tu, “Wewe u—wewe si mnafiki, lakini uko tu makosani. Wewe uko tu makosani kwa kutokujua, si makusudi.” Sidhani ninakosea kwa kutokujua, kwa maana Neno la Mungu linashuhudia Ujumbe wangu, Nalo linapaswa kuwaambia Huyu ni Nani. Nanyi mnanisikia nikisema dhahiri Huyu si mimi, kwa hiyo basi haina budi kuwa ni Yeye. Hiyo ni kweli? Iweni na imani katika Mungu basi. Basi angalieni huku, na mmwamini Mungu. Kama mnaweza kumwamini Mungu, Mungu atawajalia. Kama anaweza kufanya jambo hilo kama alivyofanya hapo awali, basi Yeye yungali ni Mungu. Mnaamini jambo hilo?

¹⁴⁶ Mnaamini jambo hilo? Bibi fulani anayeketi hapa mbele yangu, akiniangalia, akiwa na machozi machoni mwake, kwa unyofu. Sijui yeye ni nani, sijawahi kumwona. Mimi ni mgeni kwako. Je! unafikiri Mungu ajua siri za moyo wako, shauku zako, ama dhambi yako, ama cho chote kile? Unafikiria Yeye anajua? Unafikiri Yeye angeweza kunifunulia dhambi yako, yale uliyotenda, yale usingepaswa kufanya, ama shauku yako, cho chote kile? Kama angefanya jambo hilo, je! lingekufanya umwamini Yeye, ujue kwamba haina budi kuwa ni Yeye? Je! ungekubali jambo hilo kwamba ni Yeye? Si dhambi yako inayokusumbua; umeungama hiyo. Lakini unataka ubatizo wa Roho Wake Mtakatifu. Utampata. Nilimwona akimshukia.

147 Ili mjue ya kwamba nilikuwa nikiwangalia mwanamke huyo, yeye alikuwa ananiangalia, ninataka kuwaonyesha Roho Mtakatifu. Angalieni hapa, papa hapa juu ya maskini mwanamke huyu anayeketi hapa, moja kwa moja chini ya miguu yangu hapa. Niliposema jambo hilo, hilo ni jambo lile lile analotaka, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unaamini ya kwamba utampokea, dada? Inua mkono wako, basi. Sijapata kumwona mwanamke huyu maishani mwangu, ninavyojua.

148 Mnaona mtu huyu anayeketi hapa ameinamisha kichwa chake, ameketi pale pale, huku ukosi wake haumwenei, na kadhalika. Una ugonjwa wa kibofu. Unaamini Mungu atakuponya? Inua mkono wako kama utamkubali. Vema, Mungu na akutimizie ombi lako.

149 Kijana huyu mwanamume anayeketi papa hapa, akitaka ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unaamini Mungu atakupa Huo; bwana, huku ukiwa na kamba yako nyeupe ya tai imening'inia nyuma? Mungu atakujalia.

150 Mwanamume huyu hapa anamwombea mkewe. Yeye yuko hospitalini. Unaamini ya kwamba Mungu atamponya, ampe afya? Unaamini jambo hilo? Unaweza kulipokea.

151 Huku mkono wako ukiwa umefikia kooni mwako, unaamini Mungu anaweza kuponya ugonjwa huo wa moyo unaokusumbua, huo ugonjwa wa tumbo ulio nao? Unaketi pale, sasa hivi unaumwa. Hiyo ni kweli? Unaamini Yeye anakuponya? Basi unaweza kuupokea. Amina.

152 Mnaona ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Waulizeni hao watu, mwone kama ninawajua. Siwajui, bali Yeye anawajua. Amina. Unaona ile Nuru ukutani kule, ikining'inia moja kwa moja juu ya mtu anayeketi pale. Yeye anaugua ugonjwa wa uti wa mgongo mgongoni mwake. Hatoki hapa, anatoka Georgia. Bw. Duncan, amini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya ugonjwa huo wa mgongo. Unaamini kwa moyo wako wote? Mungu akubariki.

153 Hapa yuko mtu anayeketi huku nyuma kabisa, aliye na ugonjwa wa mgongo, akiniangalia. Mimi simjui, bali ni Bw. Thompson. Unaamini? Inuka, bwana, huko nyuma, ili kwamba. . . Mimi ni mgeni kwako. Ni kweli. Lakini unaketi pale, ukiomba. Ugonjwa wako wa mgongo umepona sasa. Yesu Kristo anakuponya.

154 "Itakuwa Nuru mnamo tu wakati wa jioni ." Hivi hamwoni, Yeye yuko hapa usiku wa leo! Yeye ni yule MIMI NIKO aliye mkuu. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini jambo hilo? Je! mmetosheka na kushawishika ya kwamba huyu ni Yesu Kristo Mwenyewe, akijitambulisha Mwenyewe katika unabii?

155 Usiwe na wasiwasi kuhusu jicho lako. Mungu huwaponya wagonjwa na wanaoteseka.

¹⁵⁶ Ni watu wangapi ambao... Ni wangapi walio hapa ndani, wagonjwa? Hebu tuone mikonu yenu. Inaonekana tu kama kwamba ni mvuto mkubwa sana na mkazo. Je! kuna mmoja wenu ninyi watu aliye na kadi za maombi? Sijui jinsi gani ningewaleta kupitia hapa. Ninataka kuwaombea, nami sijui jinsi ya kufanya jambo hilo. Mnaona vile, mkiangalia kwenye ukuta, nitaweza je kuwaingiza pale? Vipi kama ukifanya njia ya upande mmoja wa kanisa kusongamana watu, utayafunga mengine papo hapo, kila mtu amesimama kimya.

¹⁵⁷ Sikilizeni, nisikieni mimi. Je! nimeshawaambia jambo lote katika Jina la Bwana likakosa kutimia? Hiyo ni kweli? Kila kitu sikuzote kimekuwa sahihi. Sijapata kuwaomba hata senti moja ya pesa maishani mwangu, sivyo? Hata wakati mmoja. Sijapata kuchukua sadaka maishani mwangu. Siko hapa kwa ajili ya pesa. Siko hapa kuwadanganya. Niko hapa kudhihirisha Neno la Mungu la wakati huu. Nimewaambia Kweli, Naye Mungu amethibitisha kwamba ni Kweli. Sasa ninawaambia, MAANDIKO YASEMA HIVI, ya kwamba kama mwamini akiweka mikono yake juu ya wagonjwa, Yesu alisema, "Watapata afya!" Mnaamini jambo hilo? Basi, katika Uwepo wa Mungu, je! hamwamini ya kwamba atafanya jambo hilo sasa hivi?

¹⁵⁸ Sasa wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, na muishikilie tu hapo kwa muda kidogo. Sasa, usi—usiombe, wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi tu; huko nje nchini. Nami, mimi mwenyewe, ninajilaza kwenye lesu hizi. Sasa nawatakeni mniangalie kwa muda kidogo tu. Ni kitu gani Mungu hajafanya? Angalieni jinsi alivyo, vile neno ambalo tumesoma, nabii ambazo tumesimulia, ya kwamba Yesu alijitambulisha Mwenyewe kwa nabii hizo. Sasa, angalieni saa, na majuma haya matatu ya mwisho mahali ambapo tumeiweka saa tunayoishi. Angalieni yale tuliyosoma, vipi kuhusu manabii wa uongo na karibu ishara ambazo zingewapoteza walio wateule. Jinsi Neno limesdhihirishwa, jinsi mungu wa kizazi hiki alivyoipofusha kwa uongo, mioyo ya watu. Na jinsi ambavyo Mungu Mwenyewe alisema kupitia kwa nabii Zake ya kwamba mambo haya yangetukia katika Wakati huu wa Laodikia. Hakuna kitu ambacho kimeachwa bila kutimia. Mungu yuko hapa Mungu yeye yule tu aliyenena na hao watu wa Emau, aliyejitambulisha Mwenyewe kwa nabii ambazo zilitabiri juu Yake, Yeye yuko hapa usiku wa leo akiutambulisha Uwepo Wake kwa nabii zilizotabiriwa kwa ajili ya wakati huu. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaweza kuamini jambo hilo? Basi wekeaneni mikono. Usijiombee, bali kwa njia yako mwenyewe mwombe huyo mtu uliyemweka mikono, kwa sababu wao wanakuombea. Sasa angalia, usitilie shaka.

¹⁵⁹ Na sasa laiti mngalionga kile ninachoangalia! Nanyi mnajua singeweza kuwadanganya, nikisimama hapa. Kama mngeweza kuona, na imani yenu ingemvuta huyo Roho Mtakatifu aliye

mkuu aliyelea kule he—hewani, ambaye sayansi imempiga picha, na kumwona Yeye akitembea kwenye jengo hili akijaribu tu kupata mahali pa—pa kutua, akijaribu kupata mahali pa kutia nanga. Amini tu jambo hilo, ndugu yangu. Yeye amelitambulisha kwa Maandiko na kadhalika, ya kwamba ni kweli. Sasa omba kwa uaminifu kwa ajili ya huyo mtu ambaye umemwekea mikono; wao wanakuombea. .

¹⁶⁰ Mpenzi Yesu wa Nazareti, kwa kuwa, tunahisi, Bwana, kwa Neno, ya kwamba Wewe uko hapa, kwa ahadi kwamba uko hapa, “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, Nipo papo hapo katikati yao. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Huko nje kwenye mawimbi ya simu hii, naomba Roho Mtakatifu aliye mkuu aingie katika kila kusanyiko. Jalia Nuru ile ile Takatifu tunayoiangalia papa hapa kanisani, jalia imwangukie kila mmoja, na kila mtu, na jalia waponywe wakati huu. Tunamkemea adui, Ibilisi, katika Uwepo wa Kristo; tunamwambia huyo adui, ya kwamba ameshindwa na—na mateso yaliyompata badala yetu, yale mauti ya Bwana Yesu na ushindi wa ufufuo katika siku ya tatu; na ushuhuda Wake uliohibitishwa ya kwamba Yeye yuko hapa kati yetu usiku wa leo, akiwa hai, baada ya miaka elfu moja mia tisa. Jalia Roho wa Mungu aliye hai aujaze kila moyo kwa imani na nguvu, na nguvu za kuponya kutokana na kufufuka kwa Yesu Kristo, Ambaye ametambulikana sasa kwa Nuru hii kuu inayolizunguka kanisa, katika Uwepo Wake. Katika Jina la Yesu Kristo, tujalie kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

¹⁶¹ Jalia kwa ajili ya lesi hizi ambazo tumeziombea, jalia zipelekewe wagonjwa na wanaoteseka ambao zimekusudiwa. Jalia Roho Mtakatifu yule yule aliye hapa sasa akijitambulisha Mwenyewe, ajitambulishe Mwenyewe kwa kila mgonjwa ambaye hizi zitawekwa juu yake. Jalia Uwepo wa Mungu ujaze mioyo yao na imani mpaka ugonjwa wa miili yao uponywe. Jambo hili tunaliomba, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Uwepo wa Yesu Kristo na katika Jina Lake Yesu Kristo, wakati sisi watumishi wa Yesu Kristo tunapoombea jambo hilo. Amina.

¹⁶² Sasa kutoka mioyoni mwenu, mimi sijali mlikuwa na shida gani, mnaweza, kutoka moyoni mwenu, kuamini kwa moyo wenu wote ya kwamba Neno la Mungu limewapa ombi lenu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ninaamini ya kwamba, kila mkono, kama nilivyoweza kuona, uliinuliwa. Kama mnaamini jambo hilo, sasa kumbukeni, imekwisha.

¹⁶³ Ninyi mlio huko nje kwenye simu, kama mmekwisha amini kwa moyo wenu wote, wahudumu wakiwa wanawawekea mikono, na wapendwa wenu wakiwawekea mikono, kama mnaamini kwa moyo wenu wote ya kwamba imekwisha, imekwisha. Roho Mtakatifu mkuu, yuko hapa Maskanini usiku wa leo. Nilimwona akitembea juu ya watu, akajionyesha

Mwenyewe hapa ukutani, kisha akashuka juu ya mtu fulani, akashuka akaja hapa kisha akapanda kupitia jengoni, akiziweka wazi siri za mioyo, ule utambulisho wa Uwepo Wake, kuonyesha ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye yuko katikati yetu! Yeye ni Mungu, Mungu asiyeshindwa.

¹⁶⁴ Na je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, na je! si sasa inawaka, kujua ya kwamba sasa tuko katika Uwepo wa Yesu Kristo aliyefufuka, Ambaye utukufu na sifa ni Zake milele; Ambaye Ndiye chapa halisi ya Yehova Mwenyezi; Ambaye alishuka chini katika mfano wa Nguzo ya Moto katika kijiti kilichowaka moto, kuvuta usikivu wa nabii; Ambaye alishuka juu ya mlima, na kila mtu ambaye aliugusa tu aliuawa, ila Musa na Yoshua. Jinsi ambavyo Yeye aliwaongoza wana wa Israeli kupitia jangwani, katika safari yao, kama mfano wa watu wa siku hizi walioitwa watoke. Yuko hapa, kwa utafiti wa sayansi, hata alijitambulisha Mwenyewe mbele ya sayansi. Na kwa matendo yake yenyewe hasa na kwa unabii Wake wenyewe hasa, mambo ambayo yametabiriwa kwamba Yeye atayafanya siku hizi, kumfanya yeye yule jana, leo, na hata milele, yamethibitishwa kikamilifu. Hivi jambo hilo halitoshi kuifanya mioyo yetu iwake ndani yetu? Mungu awabariki.

¹⁶⁵ Sasa kwa moyo mmoja, hebu tusimame na kusema: sasa ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi na Mponya. [Kusanyiko linasema, “Sasa ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi na Mponya.”—Mh.] Na kwa neema Yake, [“Na kwa neema Yake,”] tangu sasa na kuendelea, [“tangu sasa na kuendelea,”] Ee Mungu, [“Ee Mungu,”] usiruhusu kutokuamini ko kote [“usiruhusu kutokuamini ko kote”] kuingie moyoni mwangu kamwe, [“kuingie moyoni mwangu kamwe,”] kwa kuwa nimeona [“kwa kuwa nimeona”] unabii [“unabii”] wa siku hizi [“wa siku hizi”] ukitimizwa. [“ukitimizwa.”] Ninaamini [“Ninaamini”] ya kwamba Yesu Kristo [“ya kwamba Yesu Kristo”] yu hai [“yu hai”] na yuko hapa sasa [“na yuko hapa sasa”] akithibitisha Neno Lake [“akithibitisha Neno Lake”] la saa hii. [“la saa hii.”] Zile nabii [“Zile nabii”] zilizoandikwa juu Yake [“zilizoandikwa juu Yake”] sasa zimetimia kati yetu. [“sasa zimetimia kati yetu.”] Yeye ni Mwokozi wangu, [“Yeye ni Mwokozi wangu,”] Mungu wangu, [“Mungu wangu,”] Mfalme wangu [“Mfalme wangu,”] Ni wangu Wote katika yote. [“Ni wangu katika yote.”]

¹⁶⁶ Mungu mpenzi, sikia ushuhuda wetu. Na utupe sisi, siku baada ya siku, Mkate wa Uzima. Nasi tunakutolea shukrani, Ee Mungu, kutoka vilindi vya moyo wetu. Tunakushukuru, Ewe Mwenyezi, Mungu wa manabii. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Loo, ni wakati mzuri namna gani, ni majira mazuri ya namna gani!

. . . amini tu;
 Amini tu, hebu amini tu,
 Yote yatendeka, amini tu.

Na tuimbe huo namna hii.

Sasa naamini, loo! sasa naamini,
 Yote yatendeka, sasa naamini;
 Sasa naamini, loo! sasa naamini,
 Yote yatendeka, sasa naamini.

Je! huo ndio ushuhuda wenu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa tunapoinamisha vichwa vyetu.

Hata twonane huko juu!
 Hata twonane Kwake kwema;
 Hata twonane huko juu!
 Mungu awe nanyi daima!

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Mungu Awe Nanyi*. Halafu anamwambia Ndugu Neville, “Je! unataka kusema jambo fulani?”—Mh.] Lee Vayle . . .

. . . Kwake kwema;
 Hata twonane huko juu!
 Mungu awe nanyi daima!

¹⁶⁷ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, Ndugu Vayle amesimama hapa kuturuhusu kwa maombi twende zetu. Ndugu Lee Vayle, yeye ni mwandishi wa hii Maskani hapa, wa maandiko na vitabu, na kadhalika. Ndugu mpendwa sana, yeye amekuwa pamoja nami katika mikutano mingi. Laiti ningalikuwa na nafasi kumruhusu kila mhudumu, na kuwaleta hapa na kuzungumza nao. Mnaelewa, nina hakika. Kila mhudumu, tuna furaha kuwa nanyi hapa. Waamini wote, watu wa makanisa mbalimbali, wo wote wale, tuna furaha kuwa pamoja nanyi hapa. Na kweli ni maombi yetu ya sisi kwa sisi, “Mungu awe nayi hata tutakapoonana tena.” Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mikono yetu imeinuliwa, hebu tuimbe huo tena kwa uzuri sana kwa Mungu.

Hata twonane huko juu!
 Hata twonane Kwake kwema!
 Hata twonane huko juu!
 Mungu awe nanyi daima!



MATUKIO YAKIDHIHIRISHWA NA UNABII SWA65-0801E
(Events Made Clear By Prophecy)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 1 Agosti, 1965, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2004 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org